# *Ushawishi*

Nina furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, kwa ajili ya kusanyiko hili la kupendeza la—la watu, na hasa kwa ajili ya vijana, kwa vile ninasikia kwamba ibada hii asubuhi ya leo imetengwa maalumu kwa ajili ya vijana wa Shreveport. Na huo ni wakati mzuri sana maishani mwangu, na muhimu, au ningeuita wakati mkuu, kuweza kuwazungumzia wavulana na wasichana ambao wata—watakuwepo kesho, kama kuna kesho. Kwa hiyo, tuna furaha kwa ajili ya jambo hili.

2 Ni madhehebu mangapi mbalimbali yaliyowakilishwa hapa asubuhi ya leo, katika kundi hili dogo la watu? Ningesema, Wamethodisti, inueni mikono yenu. Ndiyo kwanza nimsikie akisema hilo, "Kutoka dhehebu." Vema. Wabaptisti, inueni mikono yenu. Vema. Presbiteri? Angalieni tu. Lutheri? Pentekoste? Na—na, loo, Nazarayo? Pilgrim Holiness? Dhehebu lolote ambalo sijataja, inua mkono wako. Sijui kama kuna Wakatoliki hapa ndani, hebu tuwaone wakiinua mikono yao? Naam, unaona.

3 Kunaweza kukawa na Myahudi wa Kiothodoksi, hebu tuone mkono wako? Vema, bwana. Wakati mwingine, ninaamini, hapa si muda mrefu uliopita, mkutano wa mwisho hapa, tulikuwa na mmoja wa marabi hapa kwenye mkutano, kutoka kwa Othodoksi ya Kiyahudi, ambalo ndilo, hasa, mama wa haya yote. Mnaona, alimzaa mtoto, kanisa la Othodoksi lilizaa kanisa la Kikristo. Kutokana na Uyahudi kulikuja Ukristo.

4 Basi kwa hiyo tuna furaha sana kuwaona mmewakilishwa hapa asubuhi ya leo, kwa kanisa lenu na msimamo wenu. Pia hakika ni—ninaamini hili, kwamba—kwamba, Mungu, kama angekuja leo, angeninii—asingeuliza swali hilo. Kama sote tungekuwa tunaingia asubuhi ya leo, Yeye angewachukua tu wale walio tayari kwenda.

5 Miaka iliyopita, nilikuwa nikuchunga mifugo. Nami nilikuwa huko nje miezi michache iliyopita tena, nikasimama moja kwa moja kwenye lango, pamoja na ndugu wengine ambao ninawaona wameketi hapa asubuhi ya leo. Ndugu Welch Evans, Ndugu Banks Wood kutoka katika kanisa langu huko Jeffersonville, nasi tulipitia pengo hili ambalo nimelizungumzia sana. Nami ningeketi hapo, asubuhi nyingi, wakati walipokuwa wakiwafukuza ng'ombe kutoka kwenye...Shirika, ninii... walikuwa wakiwaingiza ng'ombe wao msituni, Msitu wa Arapaho. Shirika la Hereford la Mto Msumbufu hulisha msituni upande huu wa Mto Msumbufu, ambao unaitwa East Fork. Halafu pia kuna West Fork Msumbufu, na Mto Msumbufu wa Juu hulishia upande ule.

6 Na sasa kama ranchi yako inaweza kutoa, nafikiri, ni robota mbili za nyasi kavu sasa, kwa mwaka, unaweza kumweka ng'ombe kwa robota mbili za nyasi kavu kila mmoja. Na, bila shaka, Chama cha Wafanyabiashara kina chapa yako, na ni ng'ombe wangapi ambao chapa yako—yako—yako hushughulikia, ama ranchi yako.

7 Naye mhifadhi hana budi kusimama hapo, kuwahesabu ng'ombe hawa wakati wanapoingia ndani. Halafu basi anapaswa kuwakagua, ni chapa gani zinazoingia. Na hakuna chochote kiwezacho kuingia mle isipokuwa Herefordi halisi wa ukoo safi, maana ni Shirika la Herefordi. Si chochote ila Herefordi, Herefordi aliyesajiliwa, kwa sababu ma—ma—mafahali, na idadi fulani ya mafahali kwa idadi fulani ya ng'ombe wa kike, na kadhalika. Haina budi kuwa hivyo, maana inadumisha ukoo safi wa ng'ombe sawasawa. Na lazima awe ni Herefordi aliyesajiliwa, kuingia mle ndani.

8 Pia, mwajua, ni—nilimwangalia mhifadhi vile aliwahesabu ng'ombe wanapoingia, akiangalia. Hakuna hata wakati mmoja, nilivyowahi kumwona, alipoangalia chapa ama kukagua chapa. Kulikuwa na chapa nyingi zilizoingia, kama vile ya—ya Grimes pale, Mkuo wa Almasi, yetu ilikuwa ni Mkondo wa Uturuki, ndipo basi ya Pembe Tatu, na kadhalika, chapa mbalimbali ambazo ziliingia ndani ya msitu huo. Hakuangalia ni chapa gani waliyokuwa nayo, bali alikagua kila sikio kuhakikisha kulikuwa na kibandiko cha damu pale. Hakuna chochote ila Herefodi wa ukoo safi kilichoweza kuingia.

9 Nami nimeketi pale mara nyingi, nikawazia, "Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye Hukumu." Yeye hataangalia chapa yetu kamwe, kama sisi ni Presbiteri, Methodisti, Baptisti, au chochote tulicho, ama Pentekoste; bali ataangalia kishikizo chenye alama ya Damu, ile Ishara. Hiyo ndiyo itakayotuingiza ndani, kwa sababu hakuna chochote kiwezacho kuingia Utukufuni pasipo kuwa chini ya Damu. Kishikizo chenye alama ya Damu, kwamba tumekubali kile Mungu alichotufanyia, katika Kristo. Mnaona, hakuna—hakuna kitu tuwezacho kujifanyia wenyewe, sisi tumeshindwa kabisa. Hakuna njia hata kidogo. Wakati mwanadamu alipotenda dhambi, alivuka shimo kubwa kati yake na Mungu, na kuondoka. Hakuna njia ya kurudi, hata kidogo. Bali Mungu, aliye mwingi wa rehema, alikubali Kibadala. Na hicho Kibadala leo hii, kwa ajili yetu, ni Yesu Kristo. Hicho pekee ndicho Mungu atatambua, Damu ya Mwana Wake, wakati huo ukiwadia.

10 Sasa tunao wakati mzuri kwenye Maskani ya Uzima. Tulikuwa na wakati wenye utukufu jana jioni, kumwona Roho Mtakatifu akifanya kazi miongozi mwetu. Na sote tunatazamia hilo.

11 Kila mtu anatafuta kuona mahali alikotokea, na ni nini anachofanya hapa, na ni wapi anakoenda baada ya haya. Na tumekuwa na vitabu vingi vizuri vilivyoandikwa. Ndiyo kwanza nisome baadhi ya vitabu vizuri, maishani mwangu, vya filosofia ya mwanadamu na kadhalika. Bali, japo ni vizuri vitabu hivyo viwezavyo kuwa, kipo Kitabu kimoja tu kiwezacho kukwambia ulikotoka, kile ulicho, na kule unakoelekea, na hicho ni Kitabu hiki, Biblia. Nalo Neno ni Mungu. Sasa, tunakiamini Kitabu hicho, na hicho ndicho tunachotaka kusimamia, katika siku hii. Nacho kinaahidi humo ndani kwamba tunge—tungetambulishwa kuwa sisi ni akina nani, mahali tulikotoka, na kule tunakoelekea.

12 Nilikuwa nikisoma makala si muda mrefu uliopita, katika harakati za Anderson wa Church of God, mwanahistoria akiandika. Ninaamini ilikuwa katika. . .Sikumbuki hasa sasa kwamba ulikuwa ni wakati gani. Ilikuwa ni miaka mia kadhaa baada ya kifo cha Kristo; m—mmishenari alikuja Uingereza, ambao wakati huo uliitwa Nchi-ya-Malaika. Naye alikuwa akijaribu kumuongoa mfalme wa Uingereza, kwa Ukristo. Basi walikuwa wameketi karibu na moto mkubwa, nuru za moto zilikuwa zikiangazia ba—baraza, vile tungeliita leo hii. Naye huyo mtakatifu alikuwa akijaribu kumbadilisha mfalme kwa Ukristo. Ndipo shorewanda mdogo akapeperuka kuingia kwenye nuru, akazunguka kupitia kwenye nuru, na kuondoka kuingia gizani tena.

13 Nami ninaamini kwamba matukio yote ni kwa utukufu wa Mungu. Ninaamini kwamba Yeye alituahidi kwamba angefanya kila kitu kitende kazi kwa ajili ya wema kwa hao wanaompenda.

14 Ndipo mtakatifu huyo akauliza swali, "Alitoka wapi, na alienda wapi?" Alitoka kusikojulikana, na kurudi kwa njia iyo hiyo. Basi mtakatifu huyo akasema, "Biblia hii inabeba swali kama hilo, kwetu sisi, ambapo tulikuja kutoka kusikojulikana na tunarudi kusikojulikana." Basi kesho yake asubuhi, mfalme, baada ya kuichunguza usiku kucha, kwamba mtu huyo alikuwa sahihi, yeye na nyumba yake walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zao, kesho yake asubuhi. Ambao, ni yapata miaka mia tatu au mia nne, au zaidi, baada ya kifo cha mtume wa mwisho.

15 Sasa, nafikiri tukio hili asubuhi ya leo, la sisi kuja pamoja, si kuja tu hapa kula kiamshakinywa, ingawa tu—tunathamini hilo. Sikuja kwa sababu. . .Nilikuwa nimechoka, na sikuamka kwa wakati ufaao. Nilichelewa sana. Lakini nafikiri tukio hili ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

16 Sasa hebu sisi, kwa wakati huu, tusome fungu asubuhi ya leo, ama tusome Maandiko kutoka kwenye Biblia, ambalo Bwana anaonekana kuweka moyoni mwangu kwa ajili ya vijana na wazee, pamoja, hasa kwa vijana wa Shreveport, ambao mkutano

huu umewekwa wakfu kwao. Hebu tusome kutoka Isaya mlango wa 6, mkipenda, kuanzia kifungu cha kwanza.

> *Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana,. . .na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.*
>
> *Juu yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.*
>
> *Wakaitana, kila mmoja na* mwenzake, *wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA* Mungu *wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.*
>
> *Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.*
>
> *Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi.*
>
> *Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu;*
>
> *Akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako,. . . uovu wako umeondolewa,. . .* dhambi *zako zimefunikwa.*
>
> *Kisha nikasikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni* nani *atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.*

17 Ninataka kuchukua somo kutoka kwenye hayo asubuhi ya leo, liitwalo: *Ushawishi*. Mnajua, ingawa huenda tusitake kuamini hili, lakini, kila kitu tufanyacho, tunamshawishi mtu mwingine.

18 Mimi mara nyingi huhubiri kwenye mazishi. Nami kamwe sijaribu kusema mengi sana kumhusu mtu yule aliyefariki, kwa sababu hakuna haja ya kuyasema. Watu, maisha aliyo nayo mwanamume, au mwanamke, chochote kile, aliyoishi, yatanena kwa sauti kubwa zaidi kwa kusanyiko kuliko chochote nilichoweza kusema kuwahusu. Nisingebadilisha maoni yao kamwe. Maisha yao yalieleza kile walichokuwa.

19 Halafu basi kamwe hatujui kile tunachofanya, ni ushawishi gani, kile tunachofanya, kinakuwa nao juu ya wengine. Biblia ilisema, “Sisi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote.” Hiyo ni kusema, maisha yako yanasomeka kwa sauti kubwa sana kwa umma, mpaka ushuhuda wako, ukiwa tofauti na maisha yako, hauna nguvu. Ni kile ulicho ndani yako, ndicho watu husoma; si sana kile usemacho, bali kile ulicho,

unaona. Unaweza kubandika kitu juu ya mtu fulani, useme, "Hiki ni *kile*, na kadhalika," bali maisha yako yakiwa ni tofauti na yale wanayosema, ushuhuda wako wa maisha yako una sauti kubwa kuliko ushuhuda ambao mtu mwingine angeweza kusema jambo kukuhusu. Naam. Kwa hiyo shikilia tu hiyo niani, kwamba tunaleta ushawishi kila siku, na maisha unayoishi yanathibitisha ni nini kilicho ndani yako. Huwezi kubadilisha hilo. Inaakisi. Kila mtu huakisi, nje, kile alicho ndani.

20 Na tukichukua ushuhuda wa kuwa Wakristo, nafikiri ya kwamba huo ni mmoja wa mambo ya heshima kuliko yote ambayo mwanaume au mwanamke, mvulana au msichana, angeweza kufanya, angefanya. Wakati anapochukua Jina la Kristo, kwamba yeye anaenda kuwa mwakilishi wa Kristo, unapaswa kuchunguza kila hatua unayopiga, kwa sababu mtu fulani anakuangalia. Na, katika hili, inaonyesha kile ambacho Mungu amekufanyia, ndani yako.

21 Hapa si muda mrefu uliopita, kwenye da—daraja lilikuwa lijengwe huko chini Australia, nao wakaagizia watu kutoka Marekani; wasanifu wa majengo, si wasanifu wa majengo, bali wajenzi, na kadhalika, wajenga madaraja, waje na waone ikiwa wangeweza kujenga daraja linaloweza kuenea huo mlangobahari wa maji. Nao wasingeweza kupata mtu Marekani aliyeweza—aliyeweza kuichukua hiyo. La. Wakasema, "Changarawe, na kadhalika, lisingehimili." Kwa hiyo walikuwa na wito wa jumla kwa ajili ya wajenzi wa madaraja. Hakuna mmoja wao aliyeweza kuichukua.

22 Hatimaye, kampuni nzuri ya Uingereza, walikuja, nao wakaichukua ka—kandarasi hiyo baada ya yeye kupima udongo wote. Alisema angeichukua kandarasi na kujenga daraja hilo. Kwa nini? Kumbukeni, sifa yake sasa, kama mjenzi wa daraja ulimwenguni kote, iliegemea juu ya kile kazi yake ingekuwa katika daraja hilo. Haijalishi kile alichokuwa amefanya wakati uliopita, kazi hii aliyosema angeweza kufanya, ingeonyesha hasa kile alichokuwa. Wanasema kwamba alipima kila bolti, na kila—kila kijipande cha chuma kilichoingia katika daraja hilo; udongo, na kadhalika, chini, na presha ya maji juu ya udongo. Ndipo basi wajenzi wengine wote wakasimama karibu, na kusema, "Ha—halitasimama. Ha—halina budi kuporomoka." Lakini kwenye siku ya kuzinduliwa, mtu huyo aliendesha, mwenyewe, akiongoza gwaride, kwa sababu kwamba alijua kwamba kazi yake ilijaribiwa vya kutosha, nayo ingestahimili.

23 Nafikiri hilo ni jambo kuu ambalo tungeweza kuangalia katika maisha ya Ukristo. Ilibidi pawe na daraja kukingama njia kwa jamii ya wanadamu ili kuondoka katika ulimwengu huu siku moja, wala hakuna mtu aliyeweza kufanya hilo; Malaika, Malaika Mkuu, Serafi, Kerubi, hakuna kitu kingaliweza kufanya hivyo. Mungu mwenyewe alishuka, katika umbo la Mwanadamu, akaunganisha njia na kuifanya njia, na kuvuka daraja, kwanza,

kutoka kaburini kuenda Utukufuni. Na hakika ilionyesha uakisi. Kila—kila neva katika mwili Wake, kila wazo niani Mwake, kila nguvu iliyokuwa ndani Yake, ilijaribiwa na adui. Lakini alistahimili majaribu, hata kufikia mauti yenyewe, wakati alipoyashinda.

24 Mvulana huyu mdogo, Uzia, ambaye tunazungumzia habari zake asubuhi ya leo, alikuwa ni shujaa wa Isaya. Isaya, nabii kijana katika siku za Uzia, alikuwa akimtazama jamaa huyu mdogo, kwa sababu Uzia alikuwa ni mtu mashuhuri. Alitoka katika msingi m—mzuri. Baba yake na mama, wote wawili, kwa kweli walikuwa waaminio thabiti katika Mungu. Nao walikuwa wamemlea mvulana wao kumtumikia na kumheshimu Mungu.

25 Mojawepo ya upungufu mkubwa wa siku yetu hii, katika Marekani na ulimwenguni kote, ni mzazi mtauwa, kuweka ushawishi juu ya watoto wao. Wazazi wa leo hii waliziondokea kanuni za Maandiko. Walienda zaidi kwenye mitindo ya ulimwengu. Nayo makanisa yakafanya jambo lile lile. Katika kufanya hivyo, tuliilegeza, na kuleta ulimwengu ndani ya kanisa. Na hiyo ndiyo sababu tuna siku hii mashuhuri ya . . . kama nikisema hilo kwa heshima hapa mbele ya vijana hawa. Sababu ya sisi kuwa na vifuniko vingi, na kadhalika, kama wanavyoviita, na—na tabia mbaya, sanasana ni kwa sababu ya maisha ya nyumbani waliyoshawishiwa nayo, katika siku zao za mwanzoni. Mimi ningali mwaminio, kwamba, "Mlee mtoto katika njia impasayo, na anapokuwa mzee hataiacha"

26 Sasa, Uzia alikuwa ni mvulana aliyekuwa amelelewa katika aina ya uzazi hata ulimshawishi.

27 Mwangalieni mmoja wa Wamarekani wetu mashuhuri kuliko wote ninaoweza kuwazia, alikuwa Abraham Lincoln. Yeye hakika anastahili sifa zote anazopewa, na zaidi. Alikuwa na mwanzo mbaya; alizaliwa katika familia maskini, hakuwa na njia ya kupata elimu, aliandika kwenye mchanga. Tunasikia ya kwamba vitabu viwili vya pekee alivyowahi kumiliki maishani mwake, mpaka alipokuwa na yapata umri wa miaka ishirini na moja, vilikuwa ni Biblia, na Pilgrim's Progress ama labda kilikuwa ni Kitabu cha Foxe cha Wafia Imani, kilikuwa ni kimoja kati ya vitabu hivyo. Bali, mnaona, kile mtu huyo alichosoma, kiliyashawishi maisha yake.

28 Na hilo ndilo jambo lile lile leo hii. Masoko yetu yame—yamejaa utovu wa adabu na—na uchafu, kupotosha akili za watoto wetu wadogo, na halafu tunawawekea lawama juu yao. Wakati, nafikiri, mara nyingi ni yetu, sisi watu Wakristo ambao hawatasimamia na kutetea kitu kilicho sahihi, na kuamrisha vitu hivyo vitolewe kwenye rafu zetu, na kadhalika. Halafu basi katika nyumba zetu, pia, kwamba tunalegeza na kuruhusu utovu huu wote wa adabu na kadhalika kuingia nyumbani kwetu, kuwashawishi watoto.

29 Lakini Uzia alikuwa amelelewa vizuri. Naye alikuwa, tunasikia sasa, katika Mambo ya Nyakati ya Pili 26, unaweza kuisoma hadithi hiyo, kwamba katika umri wa miaka kumi na sita alifanywa mfalme, baada ya kifo cha baba yake. Naye akawa mfalme kwenye umri wa miaka kumi na sita. Kwa kuwa alikuwa na hawa wazazi watauwa, alianza moja kwa moja na ufalme wake, kufanya kile kilicho chema. Kamwe hakuyajali maoni yaliyopendwa na wengi au siasa za siku hiyo. Alimtumikia Mungu.

30 Sasa, huyo ni mtu mzuri wa kushawishiwa naye, mtu atakayetetea kile kilicho chema, katika wakati ambapo maoni yanayopendwa na wengi yanaenda kinyume, na siasa zinaenda kinyume; bali mtu atakayedumu moja kwa moja barabarani.

31 Huyu Rais mpya ambaye ndiyo kwanza achukue mamlaka. . .Rais Johnson, tangu kuuawa kwa Rais Kennedy. Wakati alipouliza, hivi majuzi, ambapo aliwaita makasisi wote kote nchini kwa ajili ya maombi, kumsaidia. Ni—nilipenda hilo katika mtu huyo. Mnaona, anamwita Mungu a—amsaidie. Nasikia kwamba yeye ni mwaminio, na anamtumainia Mungu. Kwa hiyo, tunahitaji watu kama huyo.

32 Basi tunapata kwamba Uzia, katika wakati wake, ufalme wake ulienea kote hadi Misri na nchi zote zilizo karibu, mpaka ninii yake. . . Ulikuwa mkuu sana mpaka ufalme wake ukawa wa pili baada ya ufalme wa Sulemani. Utukufu wa Bwana ulikuwa pamoja naye.

33 Huu ulitoa msaada mkubwa kwa nabii kijana, Isaya, aliyekuwa akimwangalia mtu huyu, mfalme huyu kijana, kwa sababu aliletwa kwenye ikulu katika wakati wa utawala wa huyu mfalme kijana. Basi Isaya akiwa ni nabii kijana wakati huo, na akiona jinsi Mungu alivyombariki, na kumshawishi na kumpa kitu chema. Pia tunajua kwamba mataifa yote yaliyo karibu yalilipa kodi kwake; hakukuwa na vita, na lilikuwa ni jambo kuu, funzo kwa Isaya.

34 Ndipo Isaya akapata kitu kingine hapa ndani, kwamba, jinsi Mungu atawabariki wale watakaokuwa waaminifu kwa Neno Lake na Amri Zake. Uzia aliweka mfano kwa Isaya. Na jinsi ulivyokuwa ni ufalme wenye utukufu!

35 Na sasa hapa tunaona, ambapo kwamba ushuhuda wa Mkristo, haijalishi jinsi umekuwa mashuhuri katika wakati uliopita, hauna budi kuendelea hivyo daima.

36 Uzia, alipofikia mahali ambapo alifikiria alikuwa salama, ndipo akainuliwa moyoni mwake. Alifikia mahali ambapo hakuna mtu angaliweza kumwambia chochote.

37 Kama hiyo si aina ya mfano wa wengi sana leo hii! Hata tunaipata miongoni mwa vi—vi—viongozi wetu wa Kikristo. Wanafanya kazi maisha yao yote, karibu, ili kuwa askofu fulani ama mtu fulani mashuhuri mwenye ushawishi, na, punde tu

wanapofikia mahali hapo, wanatukuka. Tunawakuta wainjilisti hudumani, ambao Mungu alibariki huduma yao, ndipo, kitu cha kwanza, wanatukuka mpaka wanafikia mahali ambapo wanajihisi ya kwamba—kwamba wako salama, kote kuzunguka watu wa—wao. Wananinii tu . . . Wamefikia mahali pale ambapo wanaweza kufanya chochote watakacho, na kuepuka nacho.

38 Ni wangapi, sijui, tunaowazia sasa hivi, wa watu mashuhuri, watumishi mashuhuri, ambao Mungu amewatumia, na hatimaye wanafikia mahali mpaka wanajisikia kwamba wanajua mengi sana kuhusu Neno la Mungu, mpaka hata hawana huo wakati wa kuomba tena. Daima ni matembezi ya kijamii, kumtembelea mtu, kwenda nje kwa chakula cha jioni. Na wakati wanaopaswa kuwa wakitumia pamoja na Mungu, peke yake, peke yake katika matayarisho ili kujitokeza katika utamu wa Roho, mbele ya kusanyiko, wako nje mahali fulani pamoja na burudani fulani. Huwezi kumtumikia Mungu na mwanadamu kwa wakati mmoja. Mtumishi wa Mungu anapaswa awe ni mtu aliyetengwa, Kwake peke yake. Laiti tungeweza tu kuwafanya watu waone hilo.

39 Halafu basi wa—wanafikia mahali ambapo wanajiweka chini ya masharti, wanapokutana na watu. Wanakutana na watu, na inabidi kuwe na hitaji la *hili* na hitaji la *lile*. Ndipo basi mtu wa Mungu anavurugika akili kabisa, na amevurugika sana anapoenda chumbani mwake. Anaanza kusoma, "Sasa nisipofanya *hili*, mtu *huyu* atasikia vibaya kuhusu hilo. Na *hili*, nisipofanya hili, mtu *huyu* atasikia vibaya kuhusu hilo." Ndipo basi anapojitokeza mimbarani, hata hajui mahali anaposimama, amevurugika akili kabisa, huku alipaswa kutumia wakati huo pamoja na Mungu. Wao si viongozi wa kijamii. Mtu wa Mungu anapaswa kujitoa kikamilifu kwa huduma ya Mungu. Nasi tunaona kwamba hilo ni vibaya sa—sana kwamba tunalo.

40 Basi jambo jingine kuu tunalopata, maana ninatambua kwamba ninazungumza na wahudumu asubuhi ya leo. Basi tunataka . . . mimi . . . tunapokuja mbele ya kusanyiko, tukijua hili, kwamba labda hatutakutana tena jinsi tulivyo asubuhi ya leo. Halafu basi mambo unayosema, Mungu anakuwajibisha kwa ajili ya hayo. Kwa hiyo lazima uje, ukiomba na kumwuliza Mungu jambo la kusema, na halafu umtegemee Yeye unapofikia mimbarani, kwa ajili ya kitu fulani kitakachowasaidia watu.

41 Sisi sote tunawajua watu, hudumani leo hii, watu mashuhuri. Baadhi yao hufikia mahali, mpaka baada ya kulileta kusanyiko lao lote kuwazunguka, wanajihisi salama sana mpaka wanawazia wanaweza hata kutenda dhambi na kupita nayo. Tumekuwa tukiwajua wahudumu wanaochukua barabara mbaya. Pia, mara nyingi, hiyo ni kwa sababu wanajisikia salama, kwamba, "Loo, watu wataniacha nipite na chochote." Watu huenda wakakuacha, ndugu yangu, bali Mungu hatakuacha. Unaona, utajibu kwa Mungu. Hupaswi kamwe kujaribu, kama mhudumu, kujaribu kudanganya masikio ya kusanyiko lako,

haijalishi jinsi wangeweza kupiga makelele ama kupaza sauti, ama kufanya yasiyofaa, au kukupigapiga mgongoni, na kusema, "Ujumbe ni wa ajabu."

42 Huna budi kuwa ni mtumishi wa Kristo, kudumu mwenye kuheshimika pamoja na Neno hilo, kwa sababu Neno hilo litajiakisi Lenyewe kupitia wewe, nawe unaenda kumshawishi mtu fulani anayetazama maisha yako. Vijana, vivyo hivyo. Wafanyabiashara, vivyo hivyo.

43 Mfalme alijikweza kwa kiburi. Alidhani alikuwa salama sana hata Mungu angemwacha apite na chochote.

44 Mvulana mdogo tineja alisema, si muda mrefu uliopita, Mkristo, alikuwa anafanya jambo fulani, alikuwa anavutiwa na kijana fulani wa roki aliyekuwa mshiriki wa kanisa lake. Nami nilikuwa nikizungumza kwenye mkutano wa Vijana Kwa ajili ya Kristo. Basi jamaa huyu mdogo akasema, kasema, "Unajua, ninavutiwa na Fulani-wa-fulani, nafikiri yeye ni mmoja wa Wakristo waaminifu kuliko wote." Naye mvulana huyu ni bingwa wa roki.

45 Nami nikasema, "Nafikiri kuna tofauti moja tu kati ya kijana huyu na Yudasi Iskariote. Hiyo ni, Yudasi alipata vipande thelathini vya fedha, naye mtu huyu amepata milolongo ya Makadilaki na mamilioni ya dola, kwa ajili ya kumsaliti Kristo."

46 Kasema, "Ungewezaje kusema jambo kama hilo, Bw. Branham? Ungewezaje kufanya hivyo?"

Nikasema, "Kwa sababu ni kweli."

47 Ushawishi huo wa kuimba nyimbo hizo za Kikristo, na mambo kama hayo, mbele za vijana, na kutoka nje ulimwenguni namna hiyo, huweka jiwe kubwa kuliko yote ya kujikwaa, zaidi ya vilabu vyote vya pombe haramu na kila kitu kingine kilichoko nchini. Ni aibu kwamba hiyo ingekuwa, hata iruhusiwe. Kanisa linapaswa kusimama na hata lisiruhusu nyimbo hizo ziimbwe na watu kama hao. Kuchukua kipaji ambacho Mungu aliwapa, na kushawishi, huku maisha yao yakinena kwa sauti kubwa kuliko maneno yao yalicho. Watu wanawezaje kufanya michezo kama hiyo afanyayo mtu huyu, na halafu asimame na kuimba nyimbo za kidini na mambo kama hayo? Huo ni upeo wa unafiki. Na tunakuta kwamba hayo huendelea miongoni mwa Wakristo, waaminio.

48 Ndipo mwanamume huyu kijana akasema, "Vema, nitakwambia kile ninachofikiria kuhusu hilo." Kasema, "Nafikiri kwamba—kwamba Mungu ananipenda sana hata ataniacha nipite na chochote."

49 Nikasema, "Kamwe hajawahi kufanya hivyo. Kamwe hangeweza kufanya hivyo. Hata Israeli, taifa Lake; hata Daudi mtu aliyeupendeza moyo Wake mwenyewe, alivuna kila punje

aliyopanda. Nawe utavuna, pia.” Kila mmoja wetu atafanya hivyo. Tunajua hilo.

50 Lakini aliinuliwa sana moyoni mwake! Sasa ninataka kulinena neno hili kwa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Aliinuliwa sana moyoni mwake, mpaka akafikiria angeweza kuchukua mahali pa mhudumu. Alijaribu kuwa mhudumu, ambalo hakuitiwa. Nami nafikiri hapo ni mara nyingi ambapo wakati mwingine watu katika viwango hivi, na makundi ya wafanyabiashara, wa—wanafikia mahali ambapo Mungu anawabariki katika biashara yao, na kuwafanya kufanikiwa, na kadhalika, mpaka wanafikia mahali hata wanafikiria wanapaswa kuhubiri Injili, pia. Na hilo ni kosa. Hilo ni kosa. Daima unapaswa kumwacha mhudumu afanye hiyo kazi ya kuhubiri, maana, kama Oral Roberts alivyosema wakati mmoja, “Ni vigumu vya kutosha kukidumisha kitu hicho kikiwa safi, kwa wahudumu, achilia mbali watu ambao hawajaitwa kwenye ofisi hiyo.” Mnaona, mnapaswa kuwa na watu pale wanaojua, na wamewekwa wakfu kwa ajili ya kazi hiyo.

51 Hii inathibitisha hilo. Kwamba, yeye, tunakuta kwamba mtu huyu, akiwa ni mtu mashuhuri, mtu mwema, mtu mwenye heshima, bali alichukua sa—sadaka, chetezo, na akaingia kwenye madhabahu ya Bwana, kufukiza uvumba mbele za Bwana, ambalo ni kwa kuhani tu aliyewekwa wakfu kufanya hivyo. Lakini aliwazia, kwa kuwa Mungu alimpenda sana, na—na Yeye alishakuwa mwema sana kwake, kwamba angeweza kuenda kufanya hivyo, kwa vyovyote vile. Ndipo kuhani akakimbia nyuma yake, na kusema, “Wewe hujateuliwa kwa ajili ya ofisi hiyo. Mungu amekataza mtu yeyote kuingia humo, Mlawi pekee aliyewekwa wakfu kwa ajili ya huduma hiyo.” Hupaswi kamwe kufanya hiyo.

52 Na hivyo ndivyo mara nyingi, kwamba, kile, nafikiri kimeingiza ulimwengu leo hii katika vurugu kama hilo, kwamba watu hutoka na kujaribu kuchukua mahali ambapo hawajateuliwa kuchukua. Inafikia mahali ambapo wa—wanajaribu kutimiza ofisi hii, nao hawajaitiwa mahali hapo.

53 Sasa tunaona ya kwamba, ingawa ni mtu mwema, aliyebarikiwa na Mungu; ila, Mungu akikubariki, wewe dumu katika kundi lile ambalo Mungu amekuita ndani yake. Kama ni mke wa nyumbani, dumu mke wa nyumbani. Kama ni katika biashara, baki katika biashara hiyo, ukimwakisi Mungu. Na chochote ambacho Mungu amekuita kwacho, acha kiwe hicho. Kwa sababu, Yeye anataka uwe mke halisi wa nyumbani, kuakisi ushawishi wako juu ya mtu mwingine ambaye angetaka kuwa mke mwema wa nyumbani. Kama wewe ni mfanyabiashara mzuri, acha maisha yako yawe kwamba yatamwakisi Yesu Kristo katika biashara yako, pamoja na uaminifu na uadilifu, pamoja na mambo ambayo kweli yana maana fulani. Kwa sababu, mtu fulani anayatazama maisha yako. Unamshawishi mtu fulani.

Mungu hana budi kuwa na mke halisi wa nyumbani. Mungu hana budi kuwa na tineja halisi shuleni. Mungu hana budi kuwa na m—m—mhudumu halisi, mfanyabiashara halisi, mtu atakayemwakisi Yeye. Kwa sababu, hapo wanaona, ndani yako, Kristo. Haijalishi kile ulimwengu mwingine wote unafanya, hicho hakina uhusiano wowote na wewe au mimi. Tunawajibika kwa Mungu kwa ajili ya maisha yetu, na kwa ajili ya ujuzi wetu na Kristo.

54 Sasa, tunakuta ya kwamba katika kujaribu kwake kuchukua mahali pa mhudumu, na mtu mwingine akimwambia kuwa yuko nje ya mahali pake, akimwambia kuwa hapaswi kufanya hivyo, yeye yuko "nje ya mahali pake," akawa hasira. Akakasirika, akakasirika sana mpaka uso wake ukageuka ukawa mwekundu.

55 Mnaona, lazima tuweze kusimama na kupokea masahihisho. Baadhi yao hawatafanya hivyo. Huwezi . . . Nimeenda kwenye mikutano na nimeketi kwenye kumbi za mikutano, halafu—halafu unasimama. Na watu wengine wanaingia na kuketi chini kwa dakika chache tu, ukisema neno moja ambalo hawakubaliani nalo, [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] wameenda, unaona, wanaenda mbio.

56 Vema, hilo, unajua kilichomtokea Hezekia akifanya hivyo, ama—ama Uzia, hasa? Mungu alimpiga kwa ukoma. Mtu huyo alikufa katika ukoma wake, ambao ni mfano wa dhambi. Asingevumilia kusahihishwa na Neno.

57 Na mara nyingi, leo hii, ni jambo lile lile. Wanasema, "Vema, dhehebu langu linaamini *hili*, nami sijali!" Mnaona? Chukua muda kulichunguza Neno. Mungu kamwe hatauhukumu ulimwengu kwa dhehebu, Yeye atauhukumu kwa Neno Lake. Nalo Neno Lake ni Kristo, naye Kristo ni Neno. Ni kitu kile kile, "jana, leo, na hata milele," Waebrania 13:8. Lakini, badala ya kujaribu kuchukua masahihisho, wanakasirika. Hawawezi kuvumilia Hilo. Wananinii tu . . .

58 Sasa hilo ndilo hasa Uzia alilofanya, mtu mwema. Unasema, "Vema, mtu huyo alikuwa ni . . ." Uzia alikuwa ni mtu mwema, pia, mtu mzuri, mtu aliyebarikiwa na Mungu. Lakini, haijalishi ilikuwa ni nini, lazima adumu mahali pake daima. Kwa sababu, Mungu alimpa fursa kuwashawishi wengine kwa kuwa mfalme mwenye haki, si kuhani. Nalo Neno lilimkataza kufanya hivyo, kwa hiyo akaingia ndani na alikuwa anaenda kutoa sadaka. Basi alipoitwa ashuke, alipewa Neno, kwamba hakupaswa kutenda jambo hilo; kwamba Mungu alikuwa amembariki katika biashara yake, na chochote kilichokuwa, bali si kujaribu kuchukua mahali pa kuhani huyu. Alikuwa nje ya Neno. Vema, alikuwa anaenda kulifanya kwa vyovyote vile, haijalishi kile yeyote alichosema.

59 Sasa huo si ndio mtazamo wa watu wengi sana leo hii? Hawatastahimili masahihisho ya Neno. Na hiyo ndiyo

sababu tunajikuta wenyewe tumefungamanishwa katika Baraza kubwa la Makanisa hapa, bila kujua tunakoenda, tukielekea ulimwenguni. Makumi ya maelfu ya washiriki wakiongezwa kila mwaka, nasi hatuoni mkono wa Mungu mahali popote ukisonga. Umekufa, baridi, kile hasa tu Biblia ilichosema wangekuwa, "Wakati wa kanisa la Laodikia, vuguvugu, uliotemwa kutoka kinywani mwa Mungu." Kristo akiwa nje, akijaribu kuingia ndani, nalo kanisa ndani halitamruhusu kuingia; inaonyesha picha ya leo, hasa. Kwa sababu, wanadamu hawaelewi kwamba mahali pao hutoka katika Neno, Neno la Mungu.

60 Naye Uzia alipaswa kuwa amechukua tahadhari hiyo. Sasa, kumbukeni, tunamwita, leo hii, Mkristo aliyebarikiwa na Mungu. Hakuwa tu mtu fulani wa kawaida. Alikuwa ni mtu aliyebarikiwa na Mungu, bali hakutaka kuvumilia masahihisho. Haijalishi ni kiasi gani Neno lilisema ni hivyo, yeye hakutaka kuelewa Hilo, kwa sababu alijihisi salama vya kutosha hata Mungu angeweza kumwacha apite na kitu kingine.

61 Na hiyo ndiyo shida na watu wetu leo hii kote ulimwenguni, kwamba wanawazia kuwa Mungu atawaacha wapite na kitu kilicho kinyume na Neno hili. Kamwe hatafanya hivyo. Hatuna budi kurudi kwenye masahihisho, na tuvumilie kusahihishwa na Neno. Na kwa sababu ya njia yake ya kiburi alivyotenda, hakuzingatia yale mhudumu huyu aliyosema. Angefanya yale aliyotaka kufanya. Wazia tu, sasa hebu simamisha tu hilo niani mwako kwa dakika moja.

62 Mtoto anawezaje kumkabili baba na mama, walio watauwa; tineja angewezaje kumwangalia maskini mama mtauwa usoni, huku nywele zake zikiingia mvi; na kumwambia huyu tineja, "Kipenzi, mama amekulea katika njia tofauti"? Nawe unaona huko nyuma kupitia maisha, yalichomfanyia mama. Usifanye hivyo, na kuwa jeuri na kusema, "Chukua dini yako, na uende, nitafanya nitakalo." Ni nini matokeo ya huyo tineja, ni nini kinachowafanyikia? Imekwisha. Wamepotea, kiroho, kimaadili, mara nyingi kimwili na kiakili. Wametengwa kabisa na rehema. Vema, basi, hicho kingekuwa ni kitu cha kutisha kwa mvulana au msichana tineja.

63 Basi wazia kuhusu mwanamume au mwanamke, chini katika huduma, au Mkristo anayejiita mtoto wa Mungu, na kutazama Amri za Mungu, na kugeuza mgongo wao, na kusema, "Dhehebu langu haliamini Hilo namna hiyo."

64 Tunahitaji Wakristo wenye ushawishi, wanaoshawishiwa na Neno la Mungu. Wanaume na wanawake walioitwa, kwa ajili—kwa ajili ya ushawishi kwa Kanisa teule kwa siku za mwisho, ndilo tunalohitaji. Mungu, tujalie hilo! Na watakuwepo. Wanaenda kuwepo.

65 Tunaona kwamba Uzia, kwa sababu ya kiburi chake, alipigwa kwa ukoma. Kamwe hakuwahi kupona. Hakupona.

Ilimbidi kujitenga mwenyewe kutoka katika Uwepo wa Mungu, na kufa katika nyumba ya ukoma.

66 Loo, mstari huo, mpaka, mstari huo ambapo wanaume na wanawake wanaweza kuvuka kwa urahisi! Mstari huo ambao mvulana au msichana tineja anaweza kuvuka, kati ya hukumu na rehema. Sisi sote! Mstari ambao wafanyabiashara wanaweza kuvuka! Yeyote kati yetu anaweza kuuvuka, kati ya mema na mabaya. Pia, kumbukeni, Neno la Mungu daima ndilo kitu kilicho sahihi. "Acha neno la kila mtu liwe ni uongo, bali Langu liwe Kweli," kasema Mungu.

67 Sasa, alipigwa. Ndipo wakati kijana Isaya alipoona haya, ni funzo jinsi gani hilo lilikuwa kwake wakati huo! Kuona kwamba, mtu anayeondoka mahali pake, kijana au mzee, yule anayeondoka mahali pake hana budi kupatwa na matokeo yake. Haijalishi ni kiasi gani Mungu alikuwa amembariki, angali alipatwa na matokeo yake.

68 Sasa Isaya alijifunza kwa hili, funzo kubwa. Kitu gani? Kwamba Mungu humwagiza mtu Wake kuingia mahali pake.

69 Mtu huwezi kujiagiza mwenyewe kuwa mahali fulani. Mungu hana budi kuagiza mahali pako. Usisahau hilo. Mungu hukuagiza mahali pako, na hapaswi kamwe (hata) kujaribu kuchukua mahali pa mwingine. Usijaribu kuwa kitu usicho.

70 Kama Mbunge Upshaw alivyosema wakati mmoja; yule aliyeponywa katika mkutano, na Bwana aliniruhusu kuona ono juu yake huko California. Alikuwa kiwete kwa miaka sitini na sita, na aliponywa mara moja, kwa rehema za Mungu. Akatupa mikongojo yake, na maskini kiti chake na kadhalika. Alikuwa moja kwa moja hapa Shreveport, nafikiri, na akishuhudia. Daima alikuwa na msemo huu.

71 Alikuwa ni seneta, naamini, ama kitu fulani, kwa miaka mingi, na mbunge kutoka Georgia. Pia alikuwa ni mwakilishi wa kanisa la Baptisti la Baraza la Kibaptisti la Kusini. Ndipo basi—ndipo basi akaenda na kugombea Rais, kwa tiketi kavu, na akashindwa kwa sababu ya msimamo wake. Basi usiku huo . . . kamwe hata sikuwa nimesikia kuhusu mtu huyo, kamwe. Daktari Roy Davis, yule aliyeniwekea mikono kwa kuweka wakfu kwa kanisa la Baptisti ya Kimishenari, akamtuma kwangu. Basi alipokuja mkutanoni, Roho Mtakatifu pale, huku maelfu ya watu wameketi, akamwita kwa jina, na kumwambia kile alichokuwa na kumwambia kwamba Bwana alikuwa amemponya. Ndipo akaja madhabahuni, bila mikongojo, bila ukanda, bila chochote. Akainama, kwenye umri wa miaka sabini na kitu, na kugusa vidole vyake vya miguu, mbele na nyuma, amekombolewa kikamilifu. Naye alikuwa ni msemaji hodari, na alikuwa ni mtu mashuhuri. Ni kitu gani yeye . . .

72 Hili hapa tamko lake, "Huwezi kuwa kitu usicho." Hiyo inasikika kama ni mimi ninasema hilo, si mbunge. Lakini hilo

lilikuwa tu. . . Yeye alikuwa ni Mkusini, na kwa namna fulani alitumia usemi wake kwa sababu alikuwa m—mtu aliyejaribu. Naye alikuwa ni ushawishi mkuu kwa watu, na mtu mtauwa. Na akafa vivyo hivyo, miaka mingi baadaye. Wakati aliposimama kwenye vipandio vya White House, kwenye mkutano wa Billy Graham, na kuimba, "Kuegemea Kwenye Mkono Wa Milele," mbele ya watu kutoka ulimwenguni kote. Sasa unaona ninii . . .

73 Mungu humwagiza mtu Wake, na huwezi kuchukua mahali pa mwingine. Ukichukua, unafanya tu uigaji wa kimwili, na hatimaye utashindwa. Unaona, huwezi kufanya hivyo. Mungu hukuagiza mahali pako. Isaya aliona hili, kwamba asingeweza kuweka tumaini lake juu ya mtu yeyote. Hapo alikuwepo mtu mashuhuri kuliko wote waliokuweko duniani, wakati huo, mfalme ambaye ulimwengu wote ulikuwa ukimlipa kodi; lakini kwa sababu alitoka mahali pake, Isaya aliona basi kwamba asingeweza kuegemea mkono wowote wa mwanadamu, na hilo likampeleka nabii hekaluni, kuomba.

74 Ee Mungu! Laiti kanisa, laiti watu wanaojiita wenyewe Wakristo, wangeweza tu kuona hili leo hii, na lingewasukuma madhabahuni mahali fulani kuomba. Huwezi kuwa kitu usicho.

75 Ndipo tunakuta kwenye . . . katika hekalu, wakati alipokuwa katika maombi. Akiwa ni nabii, maumbile yake yalikuwa ni kuona maono. Alizaliwa hivyo, bila shaka, akiwa ni nabii. Naye alihitaji mguso kutoka kwa Mungu. Na Mungu alikuwa amemchagua ku—kuwa nabii. Ndipo lile ono hekaluni, alimwona Mfalme halisi, katika ono. Alimwona Mungu ameinuliwa juu, juu kuliko Mbingu zote, na vazi Lake kuu likaijaza dunia na mbingu na anga. Aliona Mfano halisi. Kwa maneno mengine, Mungu alisema, "Tazama juu upande *huu*, mimi ndimi Mfano wako."

76 Na laiti tungeweza tu kufanya hilo, katika huduma yetu wenyewe! Ninazungumza na wahudumu, na wafanyabiashara, utineja. Wahudumu, laiti tungaliweza tu kufanya hilo! Ningependa kuwa Billy Graham. Laiti ningalikuwa na elimu na ujuzi, ku—kuweka kitu hicho pamoja kama alivyo nayo Billy Graham. Bali siwezi kuwa Billy Graham, ila Billy Graham hawezi kuwa mimi, pia. Mnaona? Sisi, kila mmoja, tuna mahali petu katika Kristo. Basi kujaribu kumwiga Billy Graham kungeweza kuwa tu ni kitu kile kile alichofanya Uzia, kungeishia tu katika njia ile ile ya maangamizi. Kuwa tu kile ulicho, kile Mungu alichokufanya kuwa.

77 Sasa, Isaya alikuwa ni nabii, kwa hiyo anashuka kwenda hekaluni na aliona Mfano halisi, Mungu. Waangalie Maserafi wa Kimbinguni, walivyopaa kupitia hekaluni. Sasa, Serafi ni—ni neno kubwa. Hapo, si Malaika. Bali ni . . . Kile alicho, ni Mteketeza dhabihu. Ni, Yeye analo jambo la kufanya kuhusiana na upatanisho, kwa sababu Yeye hutoa dhabihu, kutengeneza

njia kwa mwenye dhambi aliyetubu, kuelekea Kiti cha Rehema. Ni mahali pa jinsi gani, juu kuliko Malaika, mkubwa kuliko Malaika! Kwa kuwa, Malaika husimama nyuma. Bali Serafi huenda mbele na dhabihu, moja kwa moja katika Uwepo wa Mungu; Mteketezaji wa ninii...M—Mwasilishaji wa maombi yaliyofanywa, Mteketezaji wa dhabihu. Na Hao walikuwa hapa, wakipitia kwenye hekalu, wakilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi." Wazia hilo, hekaluni, mbele za huyu nabii kijana!

78 Moyo wake ulivunjika. Mfalme wake alikuwa amejaribu kupachukua mahali pake, aliyejaribu kuchukua mahali pa mhudumu, na alikuwa ameshindwa kabisa na Mungu, na kupigwa kwa ukoma; na—na mfano wake aliokuwa ameangalia, mwanadamu.

79 Kamwe usimtumainie mwanadamu fulani. Sijali yeye ni nani. Kama yeye ni mtu mtakatifu, kama yeye ni mwema... Hakuna kitu kama hicho. Hebu nisahihishe hilo. Hakuna mtu mtakatifu. Hakuna kanisa takatifu. Hakuna kitu kama hicho. Ni Mungu Mtakatifu, si mtu mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu. Petro wakati mmoja alirejea, "mlima mtakatifu," juu ya Mlima wa Kugeuka Sura. Sio mlima uliokuwa mtakatifu; ilikuwa ni Mungu Mtakatifu aliyekutana nao juu ya mlima huu. Si Kanisa takatifu; ni Mungu Mtakatifu katika Kanisa hilo. Si mtu mtakatifu, bali Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani ya mtu huyo. Mwanadamu atashindwa. Yeye ameshindwa kwa kuanzia, mtu yeyote. Mtu mashuhuri kuliko wote alianguka. Kamwe usiweke tumaini lako na ninii yako...kumfanya mwanadamu fulani mfano wako. Mtazamie Mungu. Kristo ndiye Mfano wako.

80 Basi tunapata kwamba alikuwa ameondoa akili yake sasa kutoka kwa Uzia, yule mfalme aliyempenda sana. Ndipo akaangalia juu na akaona kile ambacho hana budi kufahamu, kuwa nabii; kwamba Mungu, na Mungu pekee, hutawala katika maisha ya wanadamu na katika Kanisa Lake. Basi tulimwona sasa, kile kilichotendeka.

81 Tunawaona hawa Maserafi, Wao walikuwa na mabawa sita; mawili juu ya uso wao, na mawili juu ya miguu Yao, na mawili waliruka kwayo; wakipitia hekaluni, wakilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi." Walilia mchana na usiku, kwa sababu Wako katika Uwepo wa Mungu.

82 Mnaona kile Mungu alikuwa akisema, Isaya aweze kuona? Utakatifu, usafi wa Mungu, na kicho tunayopaswa kuwa nayo katika Uwepo Wake.

83 Hebu tuchunguze ono hili kwa dakika chache tu, kabla hatujafunga. Kila mmoja wa Viumbe hivi, akiwa na mabawa sita, tunatambua. Tunaenda kuchukua mabawa haya, kwanza. "Kwa mawili alifunika uso Wake." Ni kwa nini Yeye alifanya

hivyo? Wazia hilo! Hata Maserafi watakatifu, katika Uwepo wa Mungu, inawabidi kufunika nyuso Zao takatifu, kusimama Uweponi Mwake. Ambao hawakujua dhambi, hawakutenda dhambi kamwe, kamwe, hakuna njia ya Wao kutenda dhambi, bali hata hivyo, katika Uwepo wa Mungu, walifunika nyuso Zao takatifu.

84 Halafu basi sisi, wanadamu wapatikanao na mauti, wenye dhambi, waovu, tutajaribu kupenyeza kitu ndani, na kuongezea kwenye Neno Lake na kwa kusudi Lake, na kupitisha hukumu juu ya baadhi yao wanaojaribu kufuata kile Bwana alichosema ufanye; hakuna heshima kwa Neno Lake, "Ninajua Neno linasema hivyo, 'lakini huna budi kuzaliwa mara ya pili,' ila nitakwambia kile ninachowazia!" Huna wazo lolote linalokuja. Mungu amenena, na hilo latosha.

85 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Ahadi ilikuwa ni nini, ya nini? Roho Mtakatifu aliyemwagwa. Ni nini kilichowashangaza watu? Kwa sababu waliwasikia wakinena katika lugha ambazo hawakujua, nao walikuwa wanayumbayumba kama walevi, chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Nao walikuwa wakidhihaki, wakicheka. Ndipo Petro akasema, "Ahadi ni kwa ajili yenu," wakati walipotaka kutubu, "na kwa wale walio mbali, wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu."

86 Wangapi? "Wote ambao Bwana Mungu wetu atawahi kuwaita." Sasa, huenda kanisa likakuita, dhamiri yako huenda ikakuita. Bali Mungu anapokuita, Yeye anajua jinsi ya kumvika mtumishi Wake.

87 Na watu wenye dhambi, wasomi, wenye elimu, wenye ushawishi katika madhehebu yao, wanasimama na mavazi yao ya kimadhehebu na kujaribu kuingiza kitu pamoja na hilo Neno safi, lisiloghoshiwa? Kumbukeni, Neno ni Mungu. Na ikiwa Serafi, asiyejua dhambi yoyote, ilimbidi kufunika uso Wake, kusimama katika Uwepo wa Mungu, sisi tutaonekanaje Siku ile; tutakaposimama katika Uwepo wa Neno Lake, lililohubiriwa na kuthibitishwa kikamilifu na Roho Mtakatifu, na bado tunaondoka na kusema, "Ni kuwasiliana kimawazo ama Hilo ni kitu kama hicho"?

88 Ni kitu gani kilichomfanyikia mfalme huyu, mtu mashuhuri, mwaminio, mtu aliyebarikiwa na Mungu? Alipigwa kwa ukoma, ambao ni mfano wa dhambi, kutokuamini. Hakuna tiba kwake; Kristo pekee. Naye alikufa katika hali iyo hiyo.

89 Sasa watu hawana kicho Kwake. Ni kwa nini kwamba watu hawamchi Mungu? Uchaji ulikuwa tu ni wa Mungu, umezungumziwa mara mbili katika Biblia nzima, mara zote mbili zinamhusu Mungu. Tazama, sababu hawafanyi hivyo

ni kwa kuwa hawajashawishika kikamilifu kwamba Hilo ni Mungu. Hawajashawishika kikamilifu.

90 Wala na Uzia; hakushawishika kikamilifu kwamba Mungu alitimiza kila Neno. Kwa sababu Mungu alikuwa amembariki, aliwazia, "Hilo lanitosha. Kama nimepata baraka kutoka kwa Mungu, ninaweza kufanya nitakalo."

91 Huwezi kufanya hivyo. Huwezi kufanya hivyo. Wewe, tineja, huwezi kufanya hivyo, haijalishi jinsi ulivyo maarufu, jinsi ulivyo msichana mzuri, mvulana mzuri, mcheza dansi wa kupendeza. Jinsi shule nzima inavyokuthamini, u—ulishinda elimu yako, hayo yote ni mazuri. Hakuna kitu dhidi ya hayo. Hayo ni mazuri, bali usidhanie kwamba unaweza kulikanyaga Neno la Mungu na upite nalo. Enyi wahudumu msifikirie kwamba mnaweza kufanya hivyo na kupita nalo. Hakuna mmoja wetu atakayeepuka. Enyi wake wa nyumbani, ama nyinyi wafanyabiashara, sote tunaenda kujibu kwa Mungu, kwa Neno Lake. Isaya alikuwa akijifunza hili. Hawautambui Uwepo Wake.

92 Jinsi ambavyo ingetufaidi, leo hii, kusikiliza kile Daudi alichosema. Alisema, "Bwana daima yu mbele zangu." Alizifunga Amri Zake juu ya vizingiti vya mlango na—na juu ya mwimo wa kitanda chake, na ye—yeye aliziweka kila mahali. Hata alizifunga moyoni mwake, alikusudia moyoni mwake kwamba asingetenda dhambi dhidi ya Mungu. Alidumu kila mara na Neno mbele zake. Hiyo ndiyo sababu alisema, "Sitatikisika," kwa sababu, kila kitu alichofanya, alikuwa na Neno mbele zake. Na hilo ndilo litupasalo kufanya daima, amri ya Mungu.

93 Sasa, Yeye alifunika uso Wake kwa sababu Mungu ni mtakatifu kabisa, Naye alikuwa akilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu."

94 Sasa hebu tuchukue, pili, alikuwa na vifuniko viwili vya mabawa juu ya miguu Yake. Hayo yalimaanisha nini? Unyenyekevu katika Uwepo Wake.

95 Hilo ndilo jambo gumu kwa mtu aliye na mamlaka. Hilo ndilo jambo gumu kwa msichana tineja aliye mrembo. Hilo ni jambo gumu kwa mvulana tineja aliye maarufu shuleni, mchezaji mashuhuri katika mpira wa vikapu.

96 Loo, ewe kijana, jinsi Mungu angeweza—angeweza kukutumia, kama ungalimruhusu tu kufanya hivyo! Msichana mdogo, wewe uliye na maskini sura ya kupendeza kama malkia uliyopewa na Mungu, kwa nini usitumie ushawishi huo kwa Ufalme wa Mungu, kwa kile kilichomfanya Mungu akupe hiyo, sifa hiyo ya uke. Itumie kwa njia hiyo, huna—huna budi kutokea vizuri, basi. Lakini njia yoyote nyingine, huna budi kushindwa, unaona, uta—utashindwa kabisa. Mungu alikuumba, na hakuna yeyote mwingine awezaye kuchukua mahali pako, hakuna mtu awezaye kutoshea mahali hapo. Huna budi kuwa hivyo.

97 Sasa, wanyenyekevu Mbele Zake, hawa Maserafi, wanyenyekevu Mbele Zake.

98 Kama vile Musa, wakati Musa alikuwa ni mtu mashuhuri, mwerevu, tunafahamu kwamba angeweza kuwafundisha Wamisri hekima, sayansi, na hekima kuu ya Misri.

99 Hatujawahi kuifikia bado, katika sayansi yetu. Hatujengi mapiramidi, mwajua, siku hizi. Tusingeweza kuweka moja kama ilivyo, katikati ya dunia, ambapo, haijalishi mahali jua lilipo, hakuna kivuli karibu nayo. Pia tusingeweza kujenga masfinksi, au mengi ya vitu hivyo. Na wala tusingeweza kufanya mumiani, leo hii, ambayo ingemfanya aonekane wa kawaida baada ya maelfu ya miaka. Saa chache tu ndiyo yote tunayoweza kuhifadhi maiti. Walikuwa na mafuta wakati ule, wangetumia kuhifadhi maiti, ambayo hatujui chochote kuyahusu. Rangi ambayo hata haipotezi rangi yake; nyingi ya sanaa walizokuwa nazo, na sayansi, ambazo sisi hatuna.

100 Sikilizeni, enyi vijana, unaishi katika mji wa chuo hapa, ama mji ambamo . . . nami ninaishi katika mji wa chuo kikuu. Nayo sayansi ni sawa, mradi tu haiendi nje ya Neno la Mungu. Bali, ninataka mfahamu, sayansi haiwezi ikakupa uhai. Sayansi inaweza kukuambia jinsi ambavyo . . .

101 Tena—tena jambo jingine, sayansi inabidi daima kurudisha nyuma, kikawaida, kile wanachosema kuwa kimethibitishwa kisayansi. Mwajua, ndio kwanza nione hivi majuzi, p—profesa wa sayansi akinena, kwamba sasa kwamba wamethibitisha kwamba mifupa hii wanayochimbua, na kusema ina umri wa miaka milioni mia moja. Miaka miwili iliyopita, waligundua kwamba ni maji ya chumvi ambayo mfupa huo ulikuwa ndani yake. Hakuna kitu, popote katika sayansi au chochote, kinachoweza kusema kwamba ulimwengu una umri wa zaidi ya miaka elfu sita. Mnaona? Chokaa na kadhalika katika maji vimechakaza mfupa namna hiyo, ambavyo vingeweka, kuufanya uonekane kama una umri wa miaka milioni moja. Bali sivyo. Lakini unafikiri watatangaza hilo? La, bwana. Hawataghairi kile walichosema.

102 Lakini hii hapa Biblia, ndugu yangu, dada, na ndugu yangu au dada kijana tineja, kwamba haimbidi Mungu kughairi kile alichosema, kwa sababu Hicho ni Kweli, daima ni Kweli. Ni kweli daima. Wakati Mungu aliposema chochote, hicho kinamaanisha hivyo.

103 Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi kwenye mkutano, ndipo jamaa mmoja akasema, alikutana nami nje, akasema, "Wewe ni—wewe unabwekea mti usiohusika, ewe jamaa." Kasema, "Ulisema kwamba, 'Ulimwengu hapa, una umri wa miaka elfu sita.'"

Nikasema, "Utaratibu wa ulimwengu ni kweli, miaka elfu sita."

104 Akasema, "Angalia," akasema, "Biblia ilisema, kwamba—kwamba, 'Mungu aliumba mbingu na nchi, katika siku sita.'"

Nikasema, "Hakufanya hivyo."

105 Mwanzo 1, Yeye alisema, "Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi." Kituo! Ni muda gani alifanya hivyo, sijui, hakuna mwingine ajuaye. Mungu alifanya hivyo. Hicho ni kituo. Huo ndio mwisho wa sentensi. "Na," wakati Yeye alipoanza kuitumia, "nchi ilikuwa ukiwa, na utupu, na maji yalikuwa juu ya kilindi. Na Roho wa Mungu akatembea juu ya maji." Bali katika Mwanzo 1, kasema, "Mungu aliumba mbingu na nchi, hapo mwanzo." Hayo tu. Usibishane juu yake. Ninaliamini tu. Hilo latosha. Mungu aliiumba. Si kazi yangu kujua. Nina furaha aliumba, na kuniacha niishi hapa kwa muda. Anayo nyingine mpya, ambamo mnakaa haki.

Tumaini langu halijajengwa juu ya chochote pungufu
Ila Damu ya Yesu pamoja na haki.

106 Hakuna kanuni ya imani, dhehebu, hakuna mfano wa mwanadamu; ninamtaka Kristo, na Yeye pekee. Hilo ndilo litupasalo kuwa nalo.

107 Mnyenyekevu. Musa, mtu mwenye elimu; bali katika Uwepo wa kile kichaka kilichowaka moto, alivua viatu vyake. Alikuwa mahali patakatifu. Akajinyenyekeza! Unyenyekevu. Huo ndio uliokuwa kufunikwa kwa miguu, unyenyekevu.

108 Mwangalie Paulo, yule msomi mashuhuri mwenye elimu; aliyefunzwa chini ya Gamalieli, mmoja wa walimu mashuhuri kuliko wote wa Kiebrania wa siku zake. Mwerevu, mwenye elimu, shahada ya chuoni, naye alidhania alijua yote. "Na kundi hili la watu waliokuwa wakifanya yasiyofaa walikuwa si kitu ila wendawazimu, wenye kichaa," naye alikuwa na amri kutoka kwa kuhani wake mkuu, kuenda huko chini na—na kuwatia mbaroni wote, huko chini Dameski. Basi siku moja, akiteremka barabarani, alikuja katika Uwepo wa Yule yule ambaye alinena na Musa katika kichaka kilichowaka moto, Nguzo ya Moto. Paulo alifanya nini, Sauli, hasa? Alianguka kifudifudi, kwa unyenyekevu; kutoka kwa miguu yake, kwa uso wake, katika unyenyekevu.

109 Yohana Mbatizaji alifanya nini, yule mtu ambaye Yesu alisema, "Hakujakuwako na mtu aliyezaliwa na mwanamke kama yeye, ama awezaye kulinganishwa na yeye, hadi wakati huo"? Nabii huyo mashuhuri, aliyeteuliwa na Mungu kabla ya msingi wa ulimwengu; alinenwa, miaka elfu moja mia mbili na saba kabla hajaja, ama miaka mia saba na kumi na mbili, hasa, kabla hajaja duniani, na nabii Isaya hapa. Alifanya nini alipomwona Mtu akija akitembea kuteremka kutoka kwa kusanyiko, naye akaangalia juu na kuona ule Moto ukishuka

kutoka Mbinguni, katika umbo la hua? Alilia, "Nina haja kubatizwa na Wewe."

110 "Sina budi kupungua; Yeye hana budi kuzidi." Mungu hawezi kuwa na wawili duniani kwa wakati mmoja. Ni mmoja tu aliye na ujumbe, mwajua. "Sina budi kupungua; Yeye ndiye Mjumbe. Nimekuwapo hadi wakati huu, sasa Yeye anachukua mahali pangu." Kama vile Elisha, wakati Eliya alipopaa juu na kurusha nyuma joho lake kwa Elisha; huduma yake ilimalizika, Elisha hana budi kuchukulia mahali alipoachia. "Hana budi kuzidi; mimi lazima nipungue," Yohana Mbatizaji.

111 Fahamu udogo wako. Wewe si kitu. Wewe si kitu. Jinsi ningependa kukalia hilo kwa dakika chache! Lakini, wewe si kitu. Hebu nininii. . .Hili linasikika la kukufuru na lasikika la kifidhuli.

112 Na sidhani kuwa mimbara ni mahali pa mhudumu yeyote kufanya mizaha. Ime—imekuwa ni mizaha, kufanya yasiyofaa, madoido ya Hollywood sasa. Hiyo ndiyo shida. Hollywood, kupitia televisheni, imeteka mimbara. Wanawake wetu wamesujudia mungu-mke wa mtindo wa Hollywood, muda mrefu uliopita. Na kisha mimbara ikaingia katika Hollywood, kupitia waimbaji, na kadhalika, watu wenye vipaji. Loo, jinsi huyo ibilisi alivyo mtu mjanja. Huwezi kuchanganya mafuta na maji. Hayatachanganyikana. Angalia ushawishi mkubwa ambao watu wanaweza kuwapa wengine. Na kile ufanyacho ni ushawishi.

113 Kama unataka kuona jinsi ulivyo mashuhuri, ingiza kidole chako katika kidimbwi cha maji, ama ndoo ya maji, halafu kitoe kidole chako na ujaribu kutafuta mahali ulipoweka kidole chako. Wewe si kitu.

114 Mungu anaweza kufanya kazi bila wewe, Yeye anaweza kufanya kazi bila mimi, bali sisi hatuwezi bila Yeye. Hatuna budi kuwa na Yeye, kwa kuwa Yeye ni Uzima, na Yeye pekee. Si kujua Kitabu Chake, si kujua *hiki*, au kujua *kile*, ama kujua kanuni ya imani. "Bali kumjua Yeye ni Uzima," kumjua Yeye kama Mtu, Kristo ndani yako, Neno lililofanyika mwili ndani yako. Huko ni kumjua Yeye. Wakati Yeye, wewe na Yeye, mlifanyika, mnafanyika kitu kimoja, kama nilivyosema jana usiku katika *Ile Ishara Kuu*. Yeye hana budi kuingia ndani yako. Wewe! Mungu na mwanadamu lazima wawe kitu kimoja. Unafahamu udogo wako.

115 Sasa, katika kufunga, huenda nikatumia mabawa yale mengine mawili, la tatu. Angeweza kuruka kwa mabawa haya mengine mawili. Tazama! Uso umefunikwa na utakatifu wa Mungu, na katika kicho; miguu Yake imefunikwa katika unyenyekevu; na kwa mabawa mawili angeweza kujiingiza katika matendo, kusonga. Mungu alikuwa akimwonyesha nabii Wake jinsi mtumishi aliye tayari anavyopaswa kuwa. "Acha

kumwangalia Uzia! Huu hapa mfano wako nimetuma mbele zako: funika uso wako katika uchaji, funika miguu yako katika unyenyekevu, na uingie katika matendo!” Loo, ni mfano jinsi gani! Alikuwa amemtazama Uzia kwa muda mrefu sana, na kuona ikishindwa, sasa Mungu anamwambia la kufanya, akimwonyesha mtumishi aliye tayari. Aliingia katika matendo.

116 Kama yule mwanamke kisimani, aliingia katika matendo punde tu Yesu alipomwambia kuwa alikuwa na waume watano. Mwanamke huyo alikuwa akitazamia jambo kama hilo kutokea; miaka mia nne, hakuna nabii. Ndipo, mara ghafla, anaenda kuteka maji, asubuhi moja, bila kutarajia, na hapo akakutana na kitu halisi.

117 Mungu atamweka mbele zetu, mahali fulani, wakati fulani, bila kutarajiwa. Natumai Yeye anafanya hivyo asubuhi ya leo.

118 Alimfanyia mwanamke huyo wakati yeye hakutarajia. Basi wakati Yeye alipomwambia, “Mwanamke, nipe maji ninywe,” naye akajadiliana na Yeye kuhusu maji, na Yeye hakuwa na kitu cha kuchotea. Ndipo Yeye akamfanya ajue kwamba Yeye alikuwa na maji ambayo asingekuja pale kuchota.

119 Ndipo basi wakaanza kuzungumzia ni wapi, zilizo haki za kidini, kasema, “Baba zetu waliabudu katika mlima huu. Wewe wasema, ‘Yerusalemu.’” Ndipo Yesu, baada ya kitambo . . .

120 Alikuwa ni kitu gani? Alikuwa ni Neno. Yohana Mtakatifu 1, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Waebrania, mlango wa 4, ilisema, “Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, unakata.” Halibembelezi tu na kupapasapapasa. Hukata, likienda na likirudi. Mnaona, “Hukata hata kwenye mafuta ya mfupa, na Hilo huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Hilo ni Neno, Neno lililofanyika mwili. Nalo lilikuwa hili hapa, Yeye alifanya nini? Aliwatazama na angeweza kutambua mawazo yao, kwa sababu Yeye alikuwa ni hilo Neno, na Neno lisilobadilika. Na Yeye angali ni yeye yule. Habadiliki. Sasa, tazama, katika Neno hili lisilobadilika, Yeye aliangalia moja kwa moja usoni mwa mwanamke huyu.

121 Naye huyu hapa alikuwa amesimama, kama ambavyo tungemwita leo, mwanamke mwenye sifa mbaya, kahaba wa mtaani, ama kitu fulani, labda mtoto aliyekuwa amefukuzwa na kuachiliwa na wazazi; na wengi sana wa hao leo hii. Lakini huyu hapa alikuwa mwanamke huyu tineja, mrembo, kijana, anayependeza, labda katika mwaka wake wa kumi na nane, a—angekuwa amemaliza shule ya sekondari ya juu. Na hapa alikuwa amechukua barabara mbaya, na maadili ya maisha yake yalizorota. Naye hakuwa na kitu alichoweza kushikilia, hata hivyo, m—msichana mrembo.

122 Basi anapanda kwenda kuteka maji, ndipo anakutana na Mtu pale aliyezungumza naye. Naye akasema, “Kuna ubaguzi

hapa. Hupaswi kuzungumza nami. Wewe ni Mwebrania na mimi ni mwanamke Msamaria. Na, hata hivyo, angalia kile nilicho. Kwa nini unazungumza na mimi? Unataka nini?" Mnaona, ni—ni—ni—nia yake ilikuwa mbaya.

123 Basi, mara nyingi, vipi kama mwanamke huyo angalitupa chini mtungi wa maji na kuondoka, kama vile watu wengine husimama na kuondoka kwenye mkutano kabla hawajajua? Mnaona, isingelikuwa namna hiyo.

124 Lakini kulikuwa na kitu kingine kwa hiyo mbegu teule, kwamba kulikuwa na kitu cha kuvutia katika Mtu huyu, kwa hiyo akazungumza na Yeye. Kulitokea nini? Yeye alimwambia mwanamke huyo mambo aliyofanya. Na wakati alipofanya hivyo, akamwambia mambo haya aliyofanya, mwanamke huyo alisema, "Bwana, naona kuwa Wewe U Nabii. Hunijui." Ni kwa nini alijua kwamba Huyo alikuwa ni nabii? Kwa sababu Neno lilikuwa limemjia.

125 Biblia ilisema, "Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho, ama nabii, mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake. Na iwapo yale asemayo ni kweli, basi msikieni, kwa sababu huyo ni mwakilishi Wangu, yeye ni Neno langu likidhihirishwa."

126 Ndipo mwanamke huyo akasema, "Bwana, vinginevyo, hatujawa na nabii kwa miaka mia nne. Nami naona kuwa Wewe ni Nabii. Sasa, hatuna Andiko linalosema kwamba tunapaswa kupokea nabii sasa, nje ya Masihi. Tunajua Masihi yuaja. Na hili, ambalo hiyo ni ishara ya nabii, tunajua Yeye yuaja na Yeye atayafanya mambo haya."

127 Ndipo Yesu basi, utoshelevu mkuu ukaja, Yeye akasema, "Mimi Ndiye." Amina.

128 Kitu gani? Mara moja si kuruka na kutoka mbio, "Sitasikiliza hiyo." Akafunika uso wake, "Ninakubali niko makosani." Kwa unyenyekevu akaomba, "Nipe maji haya, Bwana, nisije hapa kuchota." Mnaona ninii—mnaona ninii . . . yeye—yeye, jinsi Mungu huwavalisha watu Wake?

129 Sasa kitu gani? Yeye yuko tayari. Ndipo inafunuliwa kwake kwamba Huyo ni Masihi. Na mara akaingia katika matendo. Ati kumzuia? Usingeweza kufanya hivyo. Moja kwa moja mjini, na akasema, "Njoni mwone Mtu Ambaye aliniambia mambo niliyofanya. Tumekuwa tukimtazamia Masihi, na Huyo hapo." Na Biblia inasema kwamba watu wa mji huo waliamini kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo. Alikuwa na kitu halisi sana ambacho angeweza kuonyesha. Ushawishi wake, baada ya kukutana na Yesu Kristo na kuleta matokeo ya moja kwa moja kwamba Biblia yake, ambayo alikuwa amefundishwa, ilimwambia kile Masihi angefanya, aliwashawishi watu kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi. Miaka mia nne, hawakuwa na kitu

chochote kama hicho, "Na huyu hapa Mtu huyo." Basi ushuhuda wake, ingawa ni kahaba, ulikuwa unashawishi.

130 Loo, ewe msichana, huenda usiishi maisha ya aina hiyo. Lakini, loo, iwapo ungekutana tu na Huyu ninayenena habari zake, jinsi ushawishi wako utakavyokuwa kwa wenzako shuleni!

131 Kijana mwanaume, kama Sauli, mwenye elimu, mwerevu, ni ushawishi wa jinsi gani aliokuwa kwa ulimwengu wote wa Kikristo. Alitumwa kama mtume kwa Mataifa, wakati alipokutana na huyu Yesu katika Nguzo ya Moto, siku ile, akijua kwamba Huyo alikuwa ni Mungu yeye yule aliyewatoa watu Wake, wa Israeli kutoka Misri, Israeli kutoka Misri. Laiti ungaliweza kukutana na Mungu yuyu huyu! Hiyo ni Biblia, ikidhihirishwa, ikithibitisha kwamba Yeye ni Mungu, thibitisho Lake moja kwa moja duniani sasa, kwamba Neno Lake limefanywa lijulikane, kwa kuwa, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Ni ushawishi wa jinsi gani utakaokuwa kwa kanisa lako, kwa jamii yako, kwa wote kila mtu utakayekutana naye. Utakuwa mtu aliyebadilika. Naam. Naam, bwana.

132 Petro, alipoona na akashawishika, kwamba . . . Tunaona kwamba, alikuwa amevua usiku kucha na hakupata kitu. Alikuwa ni mvua samaki. Alijua wakati mwezi ulipobadilika, na wakati samaki walikimbia na wakati hawakukimbia. Lakini alikuwa mwema wa kutosha kuketi chini na kumsikiliza Yesu, kwa dakika chache. Yeye hakusimama na kutoka mbio. Alisimama ili kusikiliza yote. Ndipo baada ya ujumbe kumalizika, na kila kitu, kwa kuwa alikuwa mwema kutosha . . .

133 Alikuwa amevua usiku kucha na hakupata kitu. Ni Simoni wangapi waliopo hapa ndani asubuhi ya leo, ni wangapi watakaosikiza kanda hii? Simoni, mmeruka kutoka Methodisti, kuingia Baptisti, kuingia Pentekoste, kuingia Umoja, kuingia Uwili, kuingia Utatu, kuingia kila kitu, na bado hamkupata kitu. Kwa nini msikae chini na kusikiliza kwa dakika moja? Mkopeshe tu Kristo dakika chache za muda wako.

134 Liangalie Neno likija. "Simoni," sasa Yeye anamwagiza, "shusha wavu kwa ajili ya mvuo wa samaki."

135 Basi wakati aliposhika samaki, alisema, "Bwana, nimevuta juya usiku kucha. Ni zaidi ya ufahamu wangu. Siwezi kueleza vipi."

136 Wala nami siwezi kueleza jinsi ifanyavyo kazi. Sijui mitambo. Ni nguvu tendaji tu ndizo ninazojali. Sijui jinsi Yeye afanyavyo jambo hilo, bali Yeye hulitenda kwa sababu aliliahidi.

137 Akashusha wavu. Kwa sababu, alijua kama hakukuwa na samaki mle ndani, na Mungu akasema kungekuwa na samaki mle ndani, alishusha wavu, kwa vyovyote vile.

138 Unasema, “Nimekuwa madhabahuni. Nimefanya *hili*. Nimefanya *lile*. Nimejaribu. Nimekuwa juu na chini. Ni. . .” Shusha wavu. Hiyo ndiyo Amri.

139 Basi aliposhika samaki, alifanya nini? Kwanza, alipiga magoti yake, kwa kicho na heshima, na akalia, “Ondoka kwangu, Bwana, mimi ni mtu mwenye dhambi.” Ni kitu gani? Kicho, unyenyekevu.

140 Ni neno gani lililorudi? “Usiogope, Simoni, tangu sasa utakuwa mvuvi wa watu.” Katika matendo, na akafa katika matendo. Loo, jamani!

141 Yule kipofu aliyeponywa, asingeweza kueleza. Asingeeleza jinsi ilivyokuwa kwamba Yeye alifanya hilo. Pia hakujua kama Yeye alikuwa ni mwenye dhambi au la; alisema, “Ni jambo la kushangaza kwangu, kwamba enyi watu hapa, ninyi makuhani mnaniuliza mimi nini, swali hili.”

142 Wakasema, “Ni nani aliyekuponya?” Walimwuliza baba yake na mama, lakini wao wakasema. . .

143 Tayari walikuwa, makuhani walikuwa wamewaambia, “Kama mtu yeyote alihudhuria mikutano ya Yesu! Yeye ni—Yeye ni—Yeye ni Mtu mwenye kichaa. Ukihudhuria mikutano Yake, unatengwa kutoka kanisa hili. Tutakuweka. . .” Hilo ndilo Biblia ilisema. “Tutakutoa kanisani moja kwa moja, ukihudhuria mkutano huo.”

144 Bali, huyo kipofu, mnaona, mkutano ulimjia, ndipo Yesu akamponya.

145 Ndipo basi hata wazazi wake, wakihofia kupoteza hadhi yao, ya kuwa mshiriki wa kanisa hili mashuhuri la mjini, waliona aibu kusema lolote juu yake. Wakalirudisha kwa mvulana huyo, nao wakasema, “Mwulizeni, yeye ni mtu mzima. Nendeni mkamwulize jinsi ilivyotendeka. Tunajua huyo ni mwana wetu, na sisi tunajua alizaliwa kipofu, bali mimi—mimi siendi kusema lolote.” Loo, huyo anayejifanya mwaminio, vuguvugu, mkwamia mpakani!

146 Lakini mtu huyu aliyeponywa macho yake; walisema, “Ni nani aliyekuponya?”

147 Akasema, “Mmoja aitwaye Yesu wa Nazareti.” Naam, bwana! Alikuwa ameketi kwa unyenyekevu. Kazi ilikuwa imefanywa.

148 Wakasema, “Mtu huyo ni mwenye dhambi. Hatujui, hatuna shule yoyote aliyotoka. Yeye si wa madhehebu yoyote. Hana kadi ya ushirika. Hatuna uhusiano wowote na Yeye. Tunajua Yeye ni mwenye dhambi.”

149 “Vema,” akasema, “sasa, hilo ni jambo la kushangaza.” Kasema, “Mtu aliyeweza kufungua macho yangu, ambalo halijawahi kufanywa tangu mwanzo wa ulimwengu; Mtu, Mhudumu anafungua macho yangu, ambalo halijawahi

kufanywa ulimwenguni; nanyi makasisi ambao mnapaswa kujua yote ya ndani na nje ya Neno, nanyi hamjui chochote kumhusu? Hilo ni jambo la kushangaza."

150 Wakati, Biblia yenyewe ilisema kwamba, wakati Yeye akija, "Vipofu wanapaswa kuona. Vilema wataruka kama ayala." Walipaswa wawe wameona Neno lilidhihirishwa. Mnaona?

151 Lakini mvulana huyo alijua; alishakuwa huko. Alifanya nini? Alikuwa katika matendo. Alikuwa tayari, mbele ya bosi wake. Alikuwa tayari, mbele ya makuhani. Alikuwa tayari, mbele ya baraza. Alikuwa tayari kwa ajili ya chochote, kwa sababu alikuwa amemtambua Mungu, akajinyenyekeza, na kuingia katika matendo pamoja na ushuhuda wake. Mnaona, huyo ni mtumishi halisi.

152 Nguzo ya Moto inapaswa kutuweka katika matendo leo hii, vile tumeliona likithibitishwa katika Maneno ya ahadi Yake kwa ajili ya wakati huu, siku hii ya mwisho. Inapaswa kuingiza mwenendo wote wa Mungu katika matendo.

153 Lakini, shida yake ni kwamba, dhehebu letu linasema, "Sasa ngoja kidogo, Huyo hakuja kupitia kundi letu. Hilo ni Jina la Yesu. Huyo ni—huyo ni haini. Huyo ni Mbaptisti. Huyo . . ." Mnaona? Ha-ha. Mnaona? Mnaona? Hawaoni tu Hilo. Hiyo ni kweli.

154 Ishara, loo, ishara ya Kuja Kwake imekaribia. Nasi tunajua hakuna kitu duniani . . .

155 Sayansi inatuambia, "Ni dakika tatu ifike usiku wa manane," ilituambia hivyo miaka kadhaa iliyopita. Basi, lazima tuwe tu karibu, labda, muda mfupi kabla usiku wa manane. Hatujui ni wakati gani ba—baruti itakapowaka katika mrututu. Angalia uchaguzi huu unaokuja hapa kesho. Hayo ndiyo yote ingehitaji, kuwasha tu moja. Wakati skrini hiyo ya rada itakapomulika hiyo bomu ya atomiki, kila moja yazo itaachiliwa, bali Kanisa litakuwa limeenda kabla ya wakati huo. Kwa hiyo kama hilo lingeweza kutukia dakika yoyote, nalo Kanisa halina budi kuondoka kabla ya hilo kutendeka, ni mbali kiasi gani?

156 Na mambo yale hasa ambayo Yeye alisema yangetukia, huduma Yake na yale ambayo yangetendeka katika siku za mwisho, tunayaona usiku baada ya usiku, na siku baada ya siku, ikisema kwamba wakati umekaribia. Loo, tunapaswa kujinyenyekeza na kuingia katika—katika unyenyekevu na kuingia katika matendo. Hiyo ni kweli. Neno likitimizwa, linapaswa kutuingiza sote katika matendo.

157 Sisi, kama nabii Isaya, tumeona matokeo ya watu waliojiinua wenyewe, wanaosema, "Vema, sasa, kama itakuwa mahali popote, itakuwa katika dhehebu letu. Ikija kupitia Utatu, vema. Ama, ikija kupitia Umoja, vema. Ama, ikija kupitia Church of God, Methodisti, Baptisti, Katoliki, ama Presbi- . . . Yote ni sawa."

158 Nilihojiwa hapa Mexico. Ndugu Jack alikuwa pamoja nami. Ndipo mtoto mchanga akafufuliwa kutoka kwa wafu, baada ya kufa asubuhi hiyo saa tatu. Naye alifufuliwa kutoka kwa wafu, usiku huo saa tano, jukwaani, kwa ono. Ndugu Jack alikuwepo. Nilimtuma akamwombee mtoto huyo. Na huyo mama akishikilia mtoto huyo mkononi mwake, namna *hii*. Mvua ikinyesha, ikimwagika, naye alikuwa amevaa koti la Ndugu Arment. Ndipo Billy akasema, "Nimesambaza..." Ndugu, huyu rafiki ya Ndugu Espinoza, sijui ni nini...Nikamwita, "manana," kwa sababu yeye—yeye—yeye alikuwa m—mpole sana. Na kwa hiyo nikasema... Alisambaza kadi za maombi, naye Billy alisimama tu kuhakikisha kwamba hakuuza moja. Naye alizisambaza zote. Basi mwanamke huyu alikuwa na mtoto mfu. Ndipo akasema...Mbona, Billy akasema, "Sina mabawabu wa kutosha kumzuilia."

159 Ndipo nikasema, "Asingeweza kunijua. Hanijui." Usiku uliotangulia, yule mtu kipofu alipokea kuona kwake. Na mbali kama mbele ya mimbara hii, malundo tu ya makoti makuukuu na shali, na kadhalika, watu maskini. Ndipo nikasema, "Vema, Ndugu Jack, shuka uende ukamwombee mtoto huyo." Nikasema, "Asingeweza kujua tofauti kati yako na mimi." Na yeye akakimbia tu chini ya miguu ya watu hao na kuruka juu ya migongo yao, na kutembea na huyo mtoto aliyefariki. Maskini, msichana mrembo, yapata tu urefu *huu*, labda mtoto wake wa kwanza. Na alionekana kuwa katika miaka yake ya ishirini na kitu, msichana mwenye sura nzuri sana. Na kwa hiyo nikasema, "Nenda ukamwombee, Ndugu Jack, kwa sababu hatajua nani ndiye nani." Nami nikisimama pale nyuma nikizungumza kupitia mkalimani, asingeweza kujua kama mimi ndiye nilikuwa nikiwaombea wagonjwa, ama yeye ndiye.

160 Ndugu Jack akaanza kuteremka pale chini. Ndipo nikaangalia moja kwa moja mbele zangu, na hapo kulikuwako ono, maskini mtoto huyu ameketi hapa. Nikasema, "Kamwe usijali. Mlete hapa." Katika dakika chache, mtoto huyo alikuwa hai. Kuweka mikono juu yake!

161 Akaingia katika matendo, upesi sana, kwa daktari wake; pamoja na taarifa iliyotiwa sahihi, kwamba mtoto huyo alikufa ofisini mwake asubuhi hiyo, akiwa na nimonia. Na saa tano usiku huo akawa hai tena, kwa sababu huyo mama aling'ang'ania. Ilimbidi kujipenyeza ndani. Kulikuwa na kitu halisi. Kama mtu kipofu aliweza kupokea kuona kwake, mtoto wake angeweza kufufuliwa kutoka kwa wafu. Ninapenda hilo. Mungu, tupe watu zaidi namna hiyo.

162 Naye huyo mama, Mkatoliki, akija na shanga zake mkononi, nikamwambia, "Hizo hazikuhitajika," si kukosa heshima kwa jamaa huyo mdogo. Si kukosa heshima kwa hizo, bali hizo hazihitajiki.

163 Ni Mungu tunayemwamini; si desturi yoyote, si maombi ya Methodisti, ama maombi ya Presbiteri, ama kupaza sauti kwa Pentekoste. Ni Mungu tunayemwamini; si ushanga wa Katoliki, au chochote kile. Tunamwamini Mungu, Mungu aishiye, kwa Neno Lake. Nalo Neno Lake ni Mungu. Na Hilo halina budi kuzaa, kwa sababu Hilo ni mbegu.

164 Sasa, nabii basi aliona kile madhehebu yaliyojitukuza yenyewe yalichofanya. Aliona yasingeweza kuchukua mahali pa ofisi. Walipoteza msimamo wao, pamoja na kanuni zao za imani, na kadhalika. Katika kutumainia kanuni za imani, wanakubali hizo na kuwazia kuwa ndizo Hilo. Ndipo tunakuta kwamba watu kama Uzia wanajaribu kuchukua mahali pa ofisi iliyopakwa mafuta, na wao wanashindwa. Wengi wao hugeuka kuwa wendawazimu, walevi, na kadhalika; wakijaribu kuchukua mahali pa ofisi iliyopakwa mafuta, wakijaribu kuiga. Badala ya kuwa na kile wanachozungumzia, na kuitwa na Mungu kufanya, na kuchaguliwa na Mungu kukifanya; wanakimbia kuingia katika makundi makubwa na kujenga madhehebu makubwa, na watu wenye elimu, na mambo makubwa mashuhuri, na kumetameta, na kama Hollywood; na kuhubiri. "Kuja kwa Bwana kumekaribia." Tumewaona watu wakipoteza msimamo wao, kwa sababu wanajaribu kuchukua ofisi ambayo hawakukusudiwa, kama tu vile Uzia. Tumeona makanisa yakiongofu. Tumeona, katika makusanyiko yetu ya Kipentekoste, kila Umoja ukijaribu kuwaleta wa Utatu, Utatu ukijaribu kuwaleta wa Umoja, Church of God likijaribu kuleta *hawa* huku, na hawa wengine wote wakijaribu kila mmoja kupata mwingine; waongoke, kuiga, kujaribu kufanya jambo ambalo hawajaitwa kufanya.

165 Mungu alisema, "Hubirini Injili. Dhihirisheni nguvu za Roho Mtakatifu. Ishara hizi zitafuatana na wale wanaoamini."

166 Sio, "Nendeni mkaunde madhehebu, mwe na shule, na kadhalika." Sina chochote dhidi yake, lakini hiyo haichukui mahali pa ofisi hii. Pia tunaona sasa, kwamba wanaume na wanawake ambao hujaribu kuchukua ofisi hiyo iliyopakwa mafuta, wakati hawajakusudiwa kufanya hivyo, tunaona kile kinachowafanyikia.

167 Huo hapo mfano wenu, enyi wahudumu. Tunauona katika maisha ya utineja. Tunauona kila mahali. Hiyo ni, usimwangalie mwanadamu. Mwangalie Mungu. Ondoa macho yako kwa mwanadamu, yaweke kwa Mungu.

168 Si kushawishiwa, unasema, "Loo, utukufu kwa Mungu, Bwana huniambia. BWANA ASEMA HIVI, fanya *hii-na-hii*," na hiyo kamwe haitendeki. Unaona, unajaribu kuiga kitu ambacho hujui chochote kukihusu. Usifanye hivyo. Ni hatari. Utapigwa na ukoma wa kiroho, kutokuamini, madhehebu yenu; kujaribu

kujiinua, kupata unyoya katika kofia yako, kuwa mzee wa kanisa. Ikiwa . . .

169 Kuwa kama Daudi, "Afadhali niwe mkeka wa mlangoni katika nyumba ya Mungu wangu, kuliko kukaa katika mahema pamoja na waovu." Naam, mkeka wa mlangoni. "Popote Wewe utakaponiita, Bwana, nijalie niwe mkeka mzuri zaidi wa mlangoni uliowahi kuwa nao. Ikiwabidi watu kuipangusa miguu yao juu yangu, jalia niwe mkeka halisi wa mlangoni. Nitasafisha miguu, ikiwa si kingine zaidi."

170 Hilo ndilo Yesu alilofanya wakati Yeye alipokuja duniani, Yeye alifanyika mkeka wa Mungu wa mlangoni, Mwana Wake Mwenyewe. Wewe ni nani, askofu, mzee wa jimbo, wakati Yesu alifanyika mtumishi mtawadha miguu, mkeka wa mlangoni kwenye Nyumba ya Bwana? Loo, jamani! Halafu basi sisi tunadhania kuwa mkubwa fulani, kwa sababu tunayo shahada ya udaktari, tulipitia chuoni. Angalia Mfano wako, kile Yeye alichofanya. Usiangalie kile askofu kabla yako, mzee wa kanisa kabla yako, chochote namna hiyo. Huenda alikuwa ni mtu mwema. Hiyo haijalishi. Ni wewe, mwangalie Mungu.

171 Wakati alipoona matokeo, na kisha akaona yale yaliyotokea. Sasa ninafunga, jambo moja zaidi ninasema. Miguu Yake na mikono . . . Mabawa Yake yalifunika uso Wake katika kicho, miguu Yake katika unyenyekevu, na halafu mabawa Yake mawili yalimwingiza katika matendo. Wazia tu hilo, athari za hilo ono juu ya nabii! Lilifanya nini kwa nabii? Lilimwonyesha kwamba hakuna mtu, hakuna mtu . . .

172 Usiweke tumaini lako juu ya mwanadamu. Wakati mtu huyo anapoliacha Neno la Mungu, mwache mtu huyo. Unaona, wewe mwache mtu huyo. Bakia na Mungu. Mungu ni Neno.

173 Angalia kile ma—matokeo yalifanya. Sasa, ndugu wahudumu, ninataka hili liingie ndani katika mioyo yenu, nyinyi nyote. Ni nini kilichofanyika kwa nabii? Kilimsababisha nabii huyo, aliyechaguliwa kwenye ofisi kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu . . . Karama na miito havina majuto. Ilimsababishia nabii huyo . . . Vipi kuhusu mhudumu, askofu, ambaye si kitu kama nabii; mwalimu, mchungaji, ama mwinjilisti, yanapaswa kuwafanyia nini? Bali kuona ono la Bwana, kulimsababisha nabii kukiri alikuwa ni mwenye dhambi.

174 Hakujitokeza na kusema, "Naam, utukufu kwa Mungu! Haleluya, hilo ni jema vya kutosha kwangu. Mungu asifiwe, ninaenda nje." Ama, hakuinuka na kusema, "Sitasikiliza Hilo. Nilikuwa na ushawishi wa kiakili. Si kulingana na kile kasisi asemacho." La.

175 Alipata funzo kwa hilo. Aliona kile Mungu alichokuwa akijaribu kumwonyesha. Kwa nini? Mbegu ya kiroho tayari ilikuwa ndani yake, kama ilivyokuwa ndani ya yule mwanamke kisimani, kama ilivyokuwa wengine. Walichaguliwa,

walichaguliwa kimbele kwa hili. Basi aliona sababu. Alimwona Uzia katika nyumba ya mwenye ukoma, mtu mashuhuri aliyejaribu kuiga kitu fulani. Alimwona Mungu akiwa ameketi kule, na aliona jinsi Mungu alivyowavalisha watumishi Wake na jinsi Yeye alivyowatuma nje. Ikamsababisha kusema, "Mimi ni mwenye dhambi." Ndipo ukaja wakati wa kutakaswa, baada ya maungamo, "Mimi ni mwenye dhambi."

176 Nabii, mtu ambaye alishakuwa katika ikulu ya mfalme, aliyejulikana kuwa nabii. Mnanisikia? Ilimfanya huyu nabii aliyechaguliwa, ono la Bwana lilimsababisha kulia, "Ole wangu! Mimi ni mtu mwenye midomo michafu. Ninaishi miongoni mwa wa-. . . watu wenye midomo michafu. Nayo macho yangu yameona utaratibu wa Bwana." Loo, ndugu mhudumu, waweza kuona hilo? "Macho yangu yameuona utaratibu wa Bwana."

177 Ndipo kukaja kutakaswa. Huyu hapa Kerubi anakuja na kaa la moto kutoka madhabahuni, alilokuwa ametwaa kwa makoleo yake, makoleo kutoka madhabahuni, akaliweka mkononi mwake. Basi akarudisha nyuma kichwa cha Isaya, kwa sababu alikuwa tayari kuungama, na kuungama kwamba alikuwa ni mchafu, kwa sababu alikuwa amemwangalia askofu fulani ama mtu fulani kuwa mfano wake, badala ya kuangalia kumwelekea Mungu.

178 Badala ya kuangalia kuelekea Neno, wewe uliangalia kuelekea kanuni yako ya imani, ingali inakuweka nyuma, "mtu mwenye midomo michafu."

179 Ndipo Malaika akaja na Moto, akauweka juu ya midomo yake, na kusema, "Sasa wewe ni safi."

180 Angalia utaratibu. Kamwe hakumletea kitabu, katekismo. Mungu hawaandai watumishi Wake kwa vitabu na katekismo. Yeye huwaandaa watumishi Wake kwa Moto, Moto wa kutakasa, Moto kutoka madhabahuni.

181 Ndipo akalia! Wakati alipolia na kusema, "Ole wangu, kwa kuwa nimefanya kosa; nimeweka mfano wangu, tumaini langu, katika mwanadamu. Nami ninaona utaratibu wa Bwana." Ndipo akamsafisha kwa kaa la Moto.

182 Sasa, si ni ajabu jinsi mtu huyo alivyojitambua mwenyewe kuwa mwenye dhambi? Pia angalia jinsi Mungu alivyofanya punde tu alipotambua kwamba alikuwa ni mwenye dhambi. Alikiri kuwa ni mwenye dhambi, akakiri makosa yake. Na aliona kile Mungu alichofanya na jinsi alivyokifanya, jinsi alivyomtakasa kwa kaa la Moto. Si tangazo la kanuni za imani, si lu—lundo la shanga, si jambo fulani la kihistoria. Alimtakasa kwa, Moto ulio hai, wakati uliopo.

183 Nayo Biblia ilisema kwamba, "Ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Roho Mtakatifu yuyu huyu, Yesu yuyu huyu aliyekuja katika umbo la Roho Mtakatifu, kwenye Siku ya

Pentekoste, ndiye mchakato pekee wa utakaso ambayo Mungu anajua chochote kuhusu kumtakasa mtumishi Wake.

184 Aliuona utaratibu. Aliona kile mtumishi wa Mungu, aliyeandaliwa, jinsi alivyopaswa kutenda. Aliona jinsi Mungu alivyomwandaa mtumishi Wake, jinsi alivyoliweka katika utaratibu.

185 Angalia basi yafuatayo, baada ya kutakaswa, baadaye, agizo. Baada ya yeye kufanya hili, ikafuata, halafu kitu gani? Agizo. Baada ya kukiri na kutakaswa, ilikuwa ni hapo ambapo Isaya aliyetakaswa akajibu wakati Bwana alisema, "Ni nani atakayekwenda?" Kasema, "Mimi hapa, nitume mimi."

186 Kijana mwanaume na mwanamke, maisha yako mbele zako, hukufanya wewe na mimi kushuka kwenda madhabahuni, asubuhi ya leo. Hebu tuteremke twende katika nyumba ya Mungu, kwa dakika chache. Mfanyabiashara, mke wa nyumbani, mhudumu, hebu twendeni chini katika nyumba ya Mungu.

187 Kuna kasoro mahali fulani. Mnaona? Mmekuwa na mengi zaidi kupita kiasi, na uigaji mwingi wa kimwili ulimwenguni, Ukristo. Vijana, ninawahurumia. Hamjui ni njia gani ya kugeukia. Mmoja anasema *hili*, na mmoja anasema *lile*, na mmoja anasema ni "Salamu Maria," na mwingine anasema ni kitu kingine, na mmoja anasema jiunge na kanisa *hili*, na jiunge na *lile*. Yote ni uongo, kwani Mungu ameonyesha kikamilifu kwamba kitu hicho kimekufa.

188 Sasa hebu tuende chini kwa nyumba ya Mungu, katika moyo wetu, madhabahu, hebu tuangalie juu na tuone vile Yesu anavyofanana, ambaye ni Neno. Ndipo basi tunaweza kujibu, "Mimi hapa, nitume, Bwana. Nitume kwa nyumba, kuwa mke bora. Nitume shuleni, kuwa msichana tineja bora. Nitume shuleni, kuwa mvulana tineja bora. Nitume mimbarani, mhudumu tofauti. Nitume kwa biashara yangu, mfanyabiashara tofauti." Ukiona Mfano wako, Yesu Kristo!

189 Akasema, "Mimi hapa, nitume mimi," baada ya unyenyekevu wake, baada ya kuona utaratibu, jinsi Mungu anavyomweka mtumishi Wake pamoja. Jinsi Yeye anavyomwagiza; kabla ya Yeye kumwagiza, inambidi anyenyekee, awe na kicho, na katika matendo. Na hivyo basi wakati alipoona hilo, Isaya aliyetakaswa akasema, "Mimi hapa, nitume mimi."

190 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi. [Ndugu fulani ananena kwa lugha nyingine. Dada fulani anatoa tafsiri—Mh.]

> Wakati kaa la Moto lilipomgusa nabii,
> Likimfanya kuwa safi kama inavyoweza kuwa,
> Wakati Sauti ya Mungu iliposema "Ni nani
> atakayekwenda kwa ajili yetu?"
> Ndipo akajibu, "Bwana, hapa, nitume mimi."

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu upesi,
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

191 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, "Nena, Bwana Wangu."—Mh.] Liwazie sasa, tineja, wakati wakivumisha wimbo huo. Liwazie, mhudumu, mfanyabiashara, mke wa nyumbani. Tuko chini kwenye nyumba ya Bwana sasa. Angalia juu yako na uone Mfano wako, Makerubi. Wazia tu, uko kwenye mwisho wa wakati sasa. Wakati utatoweka kuingia katika Umilele, pengine leo hii. Hatujui tu kwamba ni lini. Wazia hilo.

Wapo mamilioni sasa wanaokufa, katika dhambi na aibu; (angalia mitaani)
Kisikie kilio chao cha huzuni na uchungu;
Hima, ndugu, hima ukawaokoe;
Upesi jibu, "Bwana, mimi hapa."

Loo, nena, Bwana wangu, loo, nena . . .

Limaanishe kutoka moyoni mwako sasa. Isaya, uko wapi?

. . . nami nitakujibu upesi;
Nena, Bwana wangu . . .

Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, mko wapi?

Bwana, nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

192 Je! unamaanisha hilo kweli? Wakati Yeye anaponenea moyo wako, je! utamaanisha hilo?

Nena, Bwana wangu, loo, nena, Bwana wangu,

193 Ikiwa Yeye anakunenea wakati wanapouimba, "hivi utajibu upesi," je! utainua mkono wako, useme, "Mimi, Bwana. Mimi, Bwana"? Mungu abariki.

Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu . . .

194 "Jalia niwe ushawishi, Bwana, kwa wengine. Siwezi kufanya hivyo mpaka Wewe unitakase. Mtume Malaika sasa, Bwana."

Nena, Bwana wangu; loo, nena, Bwana wangu;
Nena, nami nitajibu, nitakujibu;
Loo, nena, Bwana wangu; nena, Bwana wangu,

195 Huku mikono yenu imeinuliwa sasa.

. . . nami nitaji- . . .

Inaonyesha kuwa Yeye ananena. Sasa hebu Moto uje na kuitakasa.

. . . Bwana wangu; nena, Bwana wangu.

196 Bwana Yesu, kama wimbo unavyoimbwa, "Nena, nami nitakujibu upesi," kwa kweli madazani ya mikono imeinuliwa hapa ndani, Bwana, miongoni mwa matineja, na miongoni mwa

wazee, wahudumu, wafanyabiashara. Hakika, Bwana, Wewe ungali unanena! Mtume Malaika sasa akiwa na kaa la Moto wa kutakasa. Waandae watumishi Wako vizuri, Bwana, kwa ajili ya kazi iliyoko mbele yetu.

197 Isaya alijua, kuwa nabii, kulihitaji zaidi ya kile alichokuwa nacho, kukidhi jibu la siku hiyo. Na ndivyo kunavyohitaji zaidi ya kile tulicho nacho, Bwana, leo hii, kukabiliana na jibu. Kunahitaji Utu wa Kristo ndani yetu. Kunahitaji Yesu, Mwenyewe, kulijibu swali. Tujalie, Bwana, jalia kwamba Roho Mtakatifu, katika Utu wa Kristo . . . ama Kristo, katika Utu wa Roho Mtakatifu, aingie ndani ya kila moyo sasa hivi tu. Tutakase, Bwana, kutokana na kutokuamini kwetu. Tusafishe kutokana na kanuni zetu za imani na upumbavu wetu wa ulimwengu huu. Tutakase na huo, Bwana, na uweke Neno Lako moyoni mwetu; na kutafakari juu Yake, mchana na usiku. Jalia jibu lije, Bwana, punde tu mioyo inapotakaswa. Tujalie, Bwana. Jalia Malaika wa Mungu aguse kila mmoja wa mioyo yetu sasa, kwa hilo kaa la Moto, tunapomngojea Yeye. Tujalie, Bwana.

198 Sasa huku vichwa vyenu, na mikono yenu, mioyo yenu, kila kitu chenu, vimeelekezwa kwa Mungu, papa hapa katika hekalu la Mungu, ambapo Roho Mtakatifu yupo, na pindo la vazi Lake linalijaza jengo. Uwepo wa Utu Wake upo hapa. Hebu tupokee Hilo sasa, kama unaweza kuhisi Mungu akikugusa sasa, tunapouimba wimbo huu tena.

> Wakati kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,
> Likimfanya kuwa safi kama ilivyoweza kuwa.

199 Hebu, wakati vichwa vyetu na mioyo imeinamishwa mbele Zake sasa, tuuimbe huo tena. Na hebu muache tu Malaika wa Mungu aisafishe mioyo yetu kutokana na uovu wote na—na madoido yote ya ulimwengu. Nanyi maskini wasichana na wavulana, kutoka shule ya sekondari ya juu, humu ndani, maskini matineja wa Shreveport hapa, enyi watu wema wa Kusini hapa mliozoea kuwa na Injili ya mtindo wa kale hapa chini, mnaona ya kwamba kuna kitu fulani ambacho kanisa haliwapatii leo hii, bali Mungu anacho kwa ajili yenu. Hivi hutamruhusu Yeye autakase moyo wako sasa? Mnakaa miongoni mwa watu ambao hucheza dansi, na kila kitu kingine, na kujiita wenyewe "washiriki wa kanisa," nanyi mnaona uchafu na mambo yaliyoko katika makanisa yetu kutoka kila mahali. Kuanzia Katoliki, moja kwa . . . kanisa la kwanza lililounda dhehebu hadi la mwisho, hilo ni Pentekoste, kila mmoja wetu ana hatia. Kila mmoja wana hatia, bila kuachwa yoyote.

200 Unaona mahali ambapo tumejiingiza wenyewe? Shule zetu mashuhuri za kuwaelimisha wahudumu wetu na kadhalika, na kitu walichotupotosha kuingia ndani yake, huko nje. Hebu tutupe kitu hicho kando. Tufanye kama Paulo wa kale, "Hakuna

kimoja cha vitu hivi kiwezacho kunitikisa. Nimeshawishika kwamba hakuna kitu kilichopo, wala kitu kijacho, hakuna kitu kiwezacho kututenga na upendo huo wa Mungu ulio ndani ya Kristo. Basi tukisahau mambo hayo yaliyopita, nakaza mwendo kufikia mede ya wito wa juu katika Kristo." Loo, jamani! Amini sasa, tunapofunga macho yetu na kufungua mioyo yetu Kwake, na kusema:

Wakati kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,
Likimfanya kuwa safi kabisa,
Wakati Sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
Ndipo akajibu, "Bwana, hapa, nitume mimi."
Loo, nena, Bwana wangu, nena.

Sasa hebu tumwinulie tu mikono yetu, na kuamini hilo.

Nena, nena, Bwana, nitakujibu upesi;
Nena, Bwana wangu; nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."
Naam, nena, Bwana wangu.

201 Ombeni sasa. Nitamwuliza Ndugu Don aje hapa na kuomba pamoja nasi.

Nena, nami nitakujibu upesi.

*USHAWISHI* SWA63-1130B
(Influence)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 30 Novemba, 1963, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Captain Shreve huko Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org